Nipashe
Jumamosi Juni 10, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581337
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

## OCD afariki dunia ghafla baada ya kutoka saluni

UKURASA 4



## Mbivu na mbichi uendeshaji wa bandari bungeni

UKURASA 4




UKURASA 11

# Rais Samia aingilia kati uhaba wa dola

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Biashara (TNBC), akizungumza na viongozi mbalimbali pamoja na wafanyabiashara wakati akifungua mkutano wa 14 wa baraza hilo, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**




## IGP: Uhalifu wa mtandao, fedha pasua kichwa polisi

UKURASA 3



UKURASA 3

## Nchi tano zaonyesha nia ujenzi reli ya SGR ukanda wa Mtwara

**MICHEZO** MAYELE, SAIDO JINO KWA JINO UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# ACT Wazalendo yataka uchunguzi ofisi ya DED

**Na Julieth Mkireri,** MAGU


CHAMA cha ACT Wazalendo, kimeitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Wilaya ya Magu kufanya uchunguzi kuhusu uhamishaji wa Ofisi ya Mkurugenzi.

Kimewataka wananchi kufahamu sehemu ilikohamishiwa na endapo ikibainika aliyelipwa fidia ni kiongozi wa umma, afikishwe mahakamani kwa matumizi mabaya ya ofisi.Akizungumza katika mkutano uliofanyika Mjini Magu, Kiongozi wa chama hicho, Zitto Kabwe, alisema wananchi pia, wanatakiwa kufahamu mchakato mzima hadi kuhamishwa kwa ofisi hiyo.

"Ni lazima watu wa Magu wafahamu nchi inaendeshwa kwa mujibu wa sheria na viongozi wa umma ni lazima wajue kwamba, wana wajibu wa kuheshimu sheria zilizopo,"alisema Zitto.

Kiongozi huyo alisema kuwa Kamanda wa TAKUKURU Wilaya hiyo endapo hatachukua hatua zinazotakiwa, chama hicho kitamshtaki ngazi ya taifa ili kuchukuliwa hatua na ikiwezekana aondolewe na aletwe mwingine kufanya kazi.

Katibu wa Jimbo hilo, Robert Kitula, alisema msimu wa pamba unapofika wakulima huelezwa kwamba bei zitakuwa juu lakini wakati wa kuuza huwa kinyume chake.




Msajili wa Hazina, Nehemia Mchechu akiwa ameshika mfano wa hundi ya zaidi ya sh. bilioni 6 ambazo ni gawio kwa serikali kutoka kampuni ya Mafuta ya Puma Energy, baada ya kukabidhiwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Puma, Dk. Selemani Majige (wa pili kushoto), jijini Dar es Salaam juzi. Wengine ni Mkurugenzi Mtendaji wa Puma Energy Tanzania, Fatma Abdallah (kushoto), Mkuu wa Puma Energy Afrika, Fadi Mitri (wa pili kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Rais Samia aingilia kati uhaba wa dola

**Na Beatrice Shayo**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema serikali inakusudia kuchukua hatua mbalimbali kuhusu uhaba wa fedha za kigeni unaoikabili nchini kwa sasa.

Miongoni mwa hatua hizo ni kuhakikisha mazao yanayozalishwa nchini na watalii wanaoendelea kumiminika, wanaliingizia taifa fedha za kigeni ambazo kwa sasa uingiaji wake serikalini si wa kuridhisha.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam wakati Rais akifungua kikao cha 14 cha Baraza la Taifa la Biashara (TNBC), Rais Samia alisema uchache wa fedha za kigeni unaoendelea duniani, Tanzania inaweza kuzipata kwa haraka kupitia mazao ya kilimo.

"Wazalishaji wa mazao ya chakula sasa hivi, mpunga na mahindi ni mazao ya biashara. Zamani yalikuwa mazao ya chakula na hapa nchini tunatarajia kupitia mazao hayo tunaweza kuvuna haraka na kuuza tupate fedha za kigeni," alisema.

Rais alisema wamechukua hatua za marekebisho katika mauzo ya chakula nchi za nje na wamefanya utafiti mdogo ulioonyesha mauzo ya mpunga na mahindi na mambo mengine yanachangia kiasi gani kwenye fedha za kigeni.

"Tukaona fedha nyingi za kigeni zinakuja kwenye mazao yanayotolewa nje ya nchi na hata hayo mengine hayaleti fedha za kigeni. Wajanja wananunua ndani kwa fedha ya ndani, wao wanauza kwa fedha za kigeni ambayo hairudi tena ndani. Kwa hiyo serikali inachukua hatua kurekebisha hilo kuhakikisha mazao yanaleta fedha za kigeni ndani ya nchi," alisema.

Rais Samia alisema utalii ni moja ya sekta muhimu kwa uchumi, hivyo ni muhimu kuwapo kwa udhibiti wa fedha za kigeni ili ziingie katika uchumi.

"Mpaka sasa tumeona watalii wengi na malengo ya 2025 tunaweza kuyafikia lakini bado hatujaona fedha kuingia serikalini. Kwa hiyo tutakamatana kidogo huko ili fedha irudi serikalini. Natumaini mikononi kwenu kuna dola nyingi sana zinaingia kuliko zinazoingia serikalini. Tutawaita sekta ya utalii tukae pamoja tuone namna na ninyi mnavyoweza kuisaidia serikali kurudisha dola ndani ya nchi," alisema Rais.

Alisema kazi kubwa iliyofanyika baada ya Filamu ya The Royal Tour imewezesha kuleta watalii wengi na wanatarajia mwakani wataongezeka.

Rais alisema anatambua changamoto ni kwamba wageni wanaokuja mwakani na mwaka utakaofuata watakosa mahali pa kulala endapo hawatachangamka kujenga hoteli kwa sasa, hivyo akaitaka sekta binafsi kuchangamkia fursa hiyo.

Alisisitiza suala la utoaji wa vibali kwa taasisi zinazohusika kuhakikisha wanapunguza mlolongo wa kutoa vibali vya ujenzi vya hoteli.

"Utafiti mdogo uliofanyika wageni waliokuja mwaka jana waliorudi ni asilimia 30. Hii inaonyesha watu wanakuja lakini wanasema Tanzania haturudi tena pamoja na vivutio tulivyo navyo. Waangalie hizo kasoro ili wageni wawe wanarudi. Takwimu zinaonyesha wageni wanaotaka kuja na hofu yao ni sehemu ya kulala," alisema.

**MIFUMO KUSOMANA**

Pia alisema kazi kubwa watakayoifanya serikalini ni kuhakikisha mifumo ndani ya sekta ya umma inasomana na kuwa na vigezo vya kimataifa. Alisema changamoto zilizotajwa zikiwamo za Kariakoo zimesababishwa na mifumo.

"Si zaidi ya miezi sita ninawaahidi tutakuwa tunasoma kinachotokea bandarini nakisoma mimi Ikulu," alisema.

Kuhusu baraza hilo, alisema mategemeo yake litaendelea kuwa moja ya vyombo rasmi cha kuishauri serikali kuhusu hatua muhimu za kuboresha mazingira ya biashara kwa lengo la kujenga uchumi himilivu, shirikishi.

Alisema mashauriano hayo yawe ni njia ya kuimarisha uwezo wa sekta binafsi kuzalisha bidhaa za huduma zitakazopunguza uagizaji na kuongeza mauzo katika masoko ya kikanda na kimataifa.

Alisema hatua hiyo itasaidia nchi kupunguza matumizi ya fedha za kigeni, kuongeza mapato na kuimarisha uchumi wa nchi.

**KAULI YA TPSF**

Mwenyekiti wa Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) na Mwenyekiti mwenza wa baraza hilo, Angelina Ngalula, aliiomba serikali kuhakikisha mifumo inasomana katika kutatua changamoto zao ili kupunguza mzigo hasa kwa Mamlaka ya Mapato (TRA) kwenye usimamizi wa mapato.

Alisema wamebaini kuwa spika zinazoingizwa nchini hazina ubora unaotakiwa, hivyo kuliomba Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kufuatilia ili kupata vifaa vyenye ubora.

Ngalula alisema urasimu uzembe na kukosekana kwa ufanisi katika uendeshaji wa bandari, umekuwa ni mradi unaowapatia watu mabilioni ya fedha

Alisema TPSF inaipongeza serikali kwa hatua ngumu iliyochukua ya kukaribisha sekta binafsi katika uendeshaji wa bandari hiyo, jambo ambalo wanadhani litaongeza ufanisi, na hivyo kuharakisha ukuaji uchumi kupitia rasilimali hiyo.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI**
**IDARA YA UHAMIAJI**

**MAOMBI YA URAIA**



**Bi.EVANGELIA EVELIN GEORGE JOHN FLIAKOS** mwenye picha ilioambatanishwa kwenye barua anaomba uraia wa Tanzania kwa Mheshimiwa WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI

Yeye ni raia wa Ugiriki nchi atokayo ni Ugiriki na shughuli zake ni Mkurugenzi katika kampuni ya L**UTEGA FARM FRESH COMPANY LTD ILIYOPO Iringa.**

Ameishi nchini tangu 2008 na kwa sasa anaishi Iringa vijijini mtu yeyete mwenye sababu ya kupinga mwombaji asipewe uraia,atume taarifa yake ya maandishi iliyosainiwa kwa:

**KAMISHNA JENERALI WA UHAMIAJI, S.L.P. 1181, DODOMA.**

**KUPOTEA KWA CHETI NA RESULT SLIP**



**JACKLINE AMOSI MACHERA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne na Result slip vyenye index namba **S3648-0022** vilivyotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **THEOFLO NGOWI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2020. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/URA/RB/195189/2023**

**CHANGE OF NAME BY DEED POLL**

**BY THIS DEED MAGIDALENA MASTALA MWAMPASHI former Knows as MAGADALENA RICHARD MSABILA OF** P.o. Box 07 Ileje Do hereby absolutely renounce and abandon the use of the said name Of **MAGADALENA RICHARD MSABILA** in pursuance of such change of name And as aforesaid I hereby declare that, I will be known at all times here after in all records deed and instrument in writing and in all action and proceedings and in all dealings and transaction and upon all occasions whatsoever use and sign the said name **MAGIDALENA MASTALA MWAMPASHI** as my name in lieu of my said former name **MAGADALENA RICHARD MSABILA** renounced as aforesaid

**AND I HEREBY AUTHORISE** and request all persons to designate and address me to the assumed named of **MAGIDALENA MASTALA MWAMPASHI**

**IN WITNESS WHERE OF** I have here unto described my name of **MAGiDALENA MASTALA** MWAMPASHI on the day and in the manner herein after appearing

SIGNED AND DELIVERED by the said MAGIDALENA MASTALA MWAMPASHI who is known to me personally or identified to me by M. NYONDO the latter known to me personally this 12nd day of APRIL 20 23.

M. Mwampashi
Deponent



BEFORE ME
Name M.G. PAMBA
Signature
Box 07 ILEJE
Commissioner for Oaths/Affirmations
Date 12/04/2023

**KUPOTEA KWA VYETI**



**SALVADOR GABRIEL MWAMWAJA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0867-0176** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia PANDAHILL SECONDARY SCHOOL mwaka 2014 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0140-0554** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia MZUMBE SECONDARY SCHOOL mwaka 2017. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA **KW/RB/2609/2023**

# Nchi tano zaonyesha nia ujenzi reli ya SGR ukanda wa Mtwara

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema nchi tano zikiwamo China, Marekani na Uingereza zimeonyesha nia ya kuwekeza kwenye ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) ushoroba wa Mtwara kupitia ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP).

Nchi zingine ni Canada na Afrika Kusini na mwishoni mwa mwezi huu, serikali inatarajia kukutana na wadau hao kwa ajili ya kujadili uwekezaji huo.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete (pichani), aliyasema hayo jana wakati wa hafla ya upokeaji wa mabehewa ya ghorofa yaliyokarabatiwa kati ya 30 yatakayotumika kwenye mradi wa SGR yaliyotengenezwa na kampuni ya Lueckermeier Transport and Logistic GMBH ya Ujerumani.



"Mwishoni mwa mwezi huu tunatarajia kufanya mkutano na wadau ambao wameonyesha nia ya kujenga reli kwenye ukanda wa Mtwara," alisema. Kiongozi huyo alisema lengo la utekelezaji wa miradi hiyo chini ya PPP ni kuongeza ufanisi.

Alisema nia ya serikali ni kuhakikisha ujenzi wa miundombinu unatekelezwa PPP ili kuongeza ufanisi na kuvutia mitaji mingi kutoka sekta binafsi.

Pia alisema wanatarajia kuanza majaribio mara baada ya kichwa kuwasili mwezi ujao na hilo likikamilika wataanza rasmi safari za kipande cha kwanza cha Dar es Salaam- Morogoro.

Mwakibete alisema amerishwa nayo na kueleza kwamba kwa mara ya kwanza kwenye historia ya reli yameonekana nchini.

Alisema kinachosubiriwa sasa ni kuwasili kwa kichwa kitachovuta mabahewa hayo ambacho kinatarajiwa kuwasili nchini Julai, mwaka huu.

Mabehewa hayo ambayo ni ya ghorofa, alisema manne yana uwezo wa kubeba abiria 120 kila moja huku mengine mawili yakibeba abiria 140 kila moja.

Alisema uendeshaji wa treni hiyo kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro utarahisisha huduma za usafiri na kukuza biashara.

Mwakibete alisema serikali itaendelea kununua mabehewa mengi ili kuhakikisha usafirishaji wa bidhaa na huduma, hivyo kuchochea shughuli za kiuchumi.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema uwekezaji huo mkubwa unalenga kuleta mabadiliko katika sekta ya usafiri nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa, alisema mabehewa yaliyowasili ni daraja la kwanza na la pili.


NANGE AUCTIONMART AND DEBT COLLECTORS LTD
P.O. Box 16284-ARUSHA (HQ), TEL. 0754 748323
MANYARA BRANCH
Dealers in: AUCTIONEERS, DEBT COLLECTORS COURTBROKERS, PROPERTY VALUERS AND COMMISSION AGENTS



TANGAZO LA MNADA WA HADHARA KWA WADAIWA WA MASHIMA SACCOS

Kwa idhini tuliyopewa na **Mashima Saccos na Nanjara Reha** tutauza kwa mnada wa hadhara mali zilizoorodheshwa hapa chini ambazo ziliwekwa dhamana wakati wa kuchukua mkopo.

| S/N | JINA | DHAMANA | MAHALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|
| 1 | JOSHEPHINA KAROL | SHAMBA | ROMBO | 26 JUNE2023 Nakuendelea Saa 8:00 Mchana |
| 2 | ANJELISTA COSTA | NYUMBA | ROMBO | 26 JUNE 2023 Nakuendelea Saa 6:00 Mchana |
| 3 | PRISCUS URASA | SHAMBA | ROMBO-REHA | 26 JUNE 2023 Nakuendelea Saa 4:00 Asubuhi |
| 4 | SARAFINI MASAKI | SHAMBA | ROMBO | 28 JUNE 2023 Nakuendelea saa 4:00 Asubuhi |
| 5 | MARTINA KIMARIO | SHAMBA | ROMBO-MASHIMA | 28 JUNE 2023 Nakuendelea saa 6:00 Mchana |
| 6 | ANTIPAS MSANA | NYUMBA | ROMBO-MASHIMA | 28 JUNE 2023 Nakuendelea saa 8:00 Mchana |
| 7 | ABIUDI SAMBAYA | SHAMBA | ROMBO-MASHIMA | 30 JUNE 2023 Nakuendelea saa 6:00 Mchana |
| 8 | PIUS TESHA | SHAMBA | ROMBO-MASHIMA | 30 JUNE 2023 Nakuendelea saa 4:00 Asubuhi |
| 9 | ANATORY SILAYO | SHAMBA | ROMBO | 30 JUNE 2023 Nakuendelea saa 3 asubuhi |
| 10 | LASCO TARIMO | SHAMBA | ROMBO | 1 JULLY 2023 Nakuendelea saa 8:00 Mchana |
| 11 | MALI YA MASHIMA SACCOS | SHAMBA EKARI 2.5 | ROMBO | 1 JULLY 2023 Nakuendelea saa 6:00 JMchana |
| 12 | REGINA NGOMA | KIWANJA | ROMBO -NEYEME | 1 JULLY 2023 Nakuendelea saa 4:00 Asubuhi |

MASHARTI YA MNADA
1: Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei iliyofikiwa katika mnada, salio litalipwa ndani ya siku 14 toka tarehe yam nada huo
2: Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa mnada wa siku 14 atakuwa amepoteza haki yake mnada utarudiwa na 25% aliyolipa haitarudishwa.


# IGP: Uhalifu wa mtandao, fedha pasua kichwa polisi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Camillus Wambura, amesema moja ya mambo yanayolisumbua jeshi hilo kwa sasa, ni namna uhalifu wa mitandao na uhalifu wa kifedha unavyokua kwa kasi na unavyopangwa na kuvuka mipaka.

Amesema uhalifu huo kwa sasa, unaanza kuibuka kutokana na kukua kwa sayansi na teknolojia duniani.

Alizungumza hayo jana katika Shule ya Polisi Tanzania (TPS-Moshi), alipokwenda kuzindua ushirikiano rasmi baina ya Jeshi la Polisi na Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA).

"Kitu kikubwa hapa ni tunaongelea capacity building (kujenga uwezo) na ndiyo sasa unaona tunakwenda kuingia kwenye ushirikiano na Chuo cha Uhasibu Arusha ili kuwezesha askari, watumishi wa umma na wananchi watakaodahiliwa kujifunza mbinu za kupambana na uhalifu kwa kutumia sayansi na teknolojia ya kisasa kufanya uhalifu hasa unaovuka mipaka.

"Ni eneo nyeti sana katika dunia ya leo. Tunapoongelea uhalifu sasa hivi unaoshamiri duniani, ni uhalifu unaotokana na mipango mikubwa ya kutenda uhalifu na unaovuka mipaka.

"Tunahitaji kuwa na watumishi wetu ambao wamebobea katika kupambana na uhalifu huo," alisema.

Mkuu wa Shule ya Polisi Tanzania (TPS), Ramadhan Mungi, akitoa maelezo kuhusu ushirikiano huo, alisema wameafikiana waendeshe kwa pamoja mafunzo ya kozi fupi yanayohusu Sayansi ya Polisi, mafunzo ya kimkakati, usalama wa mtandao na mafunzo ya amani na usalama.

Aidha, alisema wamekubaliana kuendesha mafunzo ya elimu ya juu katika viwango vya shahada na shahada ya uzamili, na kwamba wamedhamiria kuanza na Shahada ya Sayansi katika Usalama wa Mtandao na Shahada ya Sayansi katika Usalama na Masoko ya Kimkakati.

Nyingine ni Shahada ya Uzamili katika Amani na Usalama na Shahada ya Uzamili katika Usalama wa Taarifa.

Kwa mujibu wa Mungi, maandalizi ya kuanzisha shahada hizo yako tayari na yataanza Oktoba 2023.

Kabla ya uzinduzi huo, Mkuu wa Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA), Prof. Eliamini Sedoyeka, alisema wameingia makubaliano ya kimkakati na Jeshi la Polisi kupitia Shule ya Polisi Tanzania (TPS) ya kutoa kozi mbalimbali zinazolenga maeneo makubwa mawili, ambayo ni ulinzi katika mtandao na eneo jingine ni mafunzo ya kimkakati ya ulinzi na usalama.

"Kozi hizo zitafundishwa katika Shule ya Polisi Tanzania na wakufunzi watatoka Chuo cha Uhasibu Arusha na wengine watakuwa wa Jeshi la Polisi," alisema Prof. Sedoyeka.


The Guardian
The Home of Great Newspaper

Our Regional Offices and Representatives




*Feel free to contact for:*
ADVERTISEMENT ON NEWSPAPERS / DIGITAL PLATFORMS AND SUBSCRIBING NEWSPAPERS / E-PAPERS

HEAD OFFICE
THE GUARDIAN LIMITED
MIKOCHENI AREA
P.o.Box 31042, Dar es salaam, Tanzania
Tel: + 255 745700710 | Email: info@guardian.co.tz

Nipashe @Nipashetz · The Guardian @Theguardiantz · IPPmedia



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo akizungumza na Balozi wa China nchini, Cheng Mingjian, katika Ofisi Ndogo ya CCM Lumumba, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbivu, mbichi uendeshaji bandari bungeni leo

**Na Restuta James**

MBIVU na mbichi kuhusu uendelezaji wa bandari utajulikana leo wakati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma (PIC), itakapowasilisha bungeni azimio la kujadili mkataba kati ya serikali ya Tanzania na Dubai.

Azimio hilo ambalo limefanyiwa pia kazi na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, litajadiliwa bungeni ili kuwapa nafasi wabunge kutoa maoni yao kabla ya kuliridhia.

Wakati hatma ya azimio hilo ikitarajiwa kujulikana leo, Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, ametaka wananchi wasikubali kupotoshwa kwa kuwa serikali iko makini kuhusu jambo hilo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Msigwa alisema Ibara ya 65 (3) (3), inaitaka serikali kuwasilisha bungeni mkataba wa ushirikiano baina yake na nchi nyingine, ili kupata maoni na ushauri wa mhimili huo.

Msigwa alisema hadi sasa serikali haijaingia mkataba wowote wa uendeshaji wa bandari isipokuwa ni huo wa ushirikiano.

"Ni mkataba ambao serikali zimekubaliana kushirikiana kuendeleza maeneo ya bandari Tanzania. Huu ni mkataba wa jumla unaosema tuko tayari kushirikiana. Kwenye mkataba huu ndiko kunatoa nafasi ya kwenda kuwa na mikataba mingine," alisema.

Alisema baada ya Bunge kuuridhia, serikali itapata nafasi ya kujadiliana na kuona maeneo ya utekelezaji na kuweka utaratibu ikiwamo muda wa mkataba.

Msigwa alisema mkataba wa ushirikiano unatoa miezi 12 kwa pande zinazohusika kuwasilisha kwenye mamlaka zingine likiwamo Bunge na kufanya majadiliano ya aina za mikataba na kwamba kinyume cha hapo, mkataba huo unakuwa umekufa.

"Kama hatukukamilisha katika miezi 12 mkataba huu unakuwa umekufa lakini baada ya kuwa mmekubaliana katika miezi 12 ndipo tutakwenda kwenye mikataba ya utekelezaji na tutaamua mikataba hiyo itakuwa ya namna gani," alisema Msigwa.

"Nataka kuwaambia Watanznaia wasikubali kupotoshwa kwa sababu wanaosema hivyo hatujui wanadhamira gani...bandari yetu ya Dar es Salaam inachangamoto ya ufanisi mdogo. Tumefanya jitihada kubwa, tumejitahidi kuongeza ufanisi wa bandari lakini ukweli kwamba bandari yetu haifanyi kwa ufanisi unaotakiwa," aliongeza.

Jana, baadhi ya vyombo vya habari vilimkariri Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Plasduce Mbossa, akisema hakuna mkataba wowote kati ya TPA na DP World kama inavyodaiwa, badala yake, kuna mkataba wa awali kati ya serikali ya Tanzania na Dubai.

Hata hivyo, alisema TPA imekuwa ikishirikiana na kampuni zingine akitolea mfano wa mkataba uliomalizika mwishoni mwa mwaka jana kati ya mamlaka hiyo na kampuni ya Hutchison kutoka Hong Kong, iliyokuwa ikiendesha gati ya makasha kupitia kampuni ya Tanzania International Container Terminal Services (TICTS) kwa miaka 22.

Mkataba unaojadiliwa kwenye Azimio la leo ni wa 'Inter- Governmental Agreement' (IGA), baina ya Serikali ya Tanzania na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), unaoeleza eneo la ushirikiano ikiwamo mafunzo, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na uendelezaji na uendeshaji wa bandari.

Ikiwa Bunge litaridhia mkataba huo, TPA itafanya majadiliano na kampuni ya DP World ya Dubai ili kuainisha maeneo ya uendeshaji wa bandari na aina za mikataba ikiwamo ukomo wake.

Kwa mujibu wa Mbossa, mikataba kati ya TPA na DP World, mwekezaji huyo atakodishiwa eneo la kufanyia shughuli zake ambazo ataziboresha kwa kuweka mitambo ya kisasa ili kuziwezesha meli kushusha mzigo ndani ya siku mbili kutoka wastani wa tisa za sasa.

# CCM, China zaahidi kukuza ushirikiano

**Na Mary Geofrey**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, na Balozi wa China nchini Tanzania, Cheng Mingjian, wamekubaliana kushirikiana, kutengeneza fursa na kubadilishana uzoefu katika sekta mbalimbali kwa manufaa ya wananchi wa mataifa hayo.

Viongozi hao walikutana jana Ofisi Ndogo ya CCM Lumumba, jijini Dar es Salaam, kujadili kuhusu kuimarisha na kudumisha urafiki na ushirikiano katika sekta za elimu, mafunzo, biashara, uwekezaji, uongozi, utawala, mapambano dhidi ya rushwa na maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano.

Makubaliano hayo yalilenga pia kuweka mbele ushirikiano unufaikaji ulio katika msingi ya usawa na maendeleo ya watu wa pande zote mbili.

"Kwa namna hadhi ya ushirikiano wa pande hizi ilivyoongezeka na kupanda, hasa kufuatia ziara ya kihistoria ya Rais Samia Suluhu Hassan, nchini China, baada ya mwaliko wa Rias wa China, Xi Jinping.

"Ni muhimu kuendelea kukutana na kuzungumza ili kuboresha, kuimarisha na kudumisha ushirikiano wetu katika nyanja mbalimbali ikiwamo kupeana fursa za mafunzo ya uongozi kwenye mambo mbalimbali, kuangalia uhusiano wa kibiashara na hata watu wa pande zote mbili," alisema Chongolo.

Balozi wa China, Mingjian aliahidi serikali ya China anayoiwakilisha inauchukulia urafiki na udugu wa pande hizo mbili kuwa wa kipekee na iko tayari kuendelea kuuenzi na kuudumisha kwa ajili ya manufaa ya watu wa nchi zote.

# OCD afariki dunia baada ya kutoka saluni

**Na Jaliwason Jasson,** SIMANJIRO

MKUU wa Polisi wa Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, (OCD), Mratibu Mwandamizi wa Polisi, Mathayo Mmari, amefariki dunia baada ya kudondoka kwenye ngazi akitoka kunyoa nywele saluni.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi (ACP) George Katabazi, akizungumza na Nipashe jana alisema: "Kifo chake ni cha kawaida alikuwa na sukari na shinikizo la damu hivyo magonjwa haya hubadilika."

Alisema wakati anatoka saluni kunyoa nywele, alianguka kwenye ngazi na kupelekwa Hospitali ya Wilaya ya Simanjiro, Orkesmet, kupatiwa matibabu ndipo umauti ulipomkuta.

Katabazi alisema wanatarajia leo mwili wake utapelekwa Mji Mdogo wa Mirerani kwa ajili ya kuagwa na baadaye utasafirishwa kwenda nyumbani kwao, Hai mkoani Kilimanjaro kwa ajili ya maziko.



Msururu wa malori yaliyobeba shehena ya mahindi yakiwa yamekwama kwenye kituo cha forodha cha Namanga, wilayani Longido mkoani Arusha jana, kwa madai ya kukiuka baadhi ya taratibu zinazotakiwa wakati wa kuvuka mpaka wa Tanzania na Kenya. **PICHA: ASRAJI MVUNGI**

# Bashe ataja sababu mkwamo malori mpakani

**Na Asraji Mvungi,** ARUSHA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amesema mkwamo wa malori ya mizigo unaoendelea kwa zaidi ya siku ya 10 sasa katika mpaka wa Namanga,, Longido mkoani Arusha, umetokana na madereva kukiuka taratibu za ukaguzi wa ubora na usalama wa chakula.

Akiwa katika Kituo cha Forodha Namanga jana, Bashe, alisema malalamiko yanayotolewa na madereva wa malori hayo hayana tija, zaidi ya kusababisha taharuki.

"Tumebaini kuwa madereva wa malori hayo wamekiuka taratibu zikiwemo za ukaguzi wa ubora na usalama wa mahindi waliyoyabeba.

"Madereva wakishirikiana na madalali, wamekiuka taratibu za ununuzi, ukiwemo wa kununua mazao kwa wakulima, ambayo hayajakauka vizuri, utaratibu ambao haukubaliki.

"Tukiruhusu mahindi hayo yakavuka mpaka kwenda nje bila kukidhi vigezo kwanza, wenzetu wa upande wa pili hawatayaruhusu yaingie. Kama yatapita kwa ujanja ujanja wa madalali yanaweza kuharibu biashara ya mazao ya Tanzania. Hivyo tutaendelea kudhibiti na kuhakikisha sheria zinafuatwa," alisema Waziri Bashe.

Kutokana na udhibiti huo, Waziri Bashe aliwataka wafanyabishara wote wa ndani na nje, kujenga utamaduni wa kuheshimu sheria na taratibu zilizoko ili kuepusha matatizo na hasara zisizo za lazima.

"Mtu yeyote anayekuja kununua mazao Tanzania, aheshimu taratibu za nchi na Watanzania wanaoshirikiana na wenzao wanaotoka nje. Tumieni vizuri fursa ya kufanya biashara popote, lakini heshimuni sheria,"alisisitiza

Kabla ya kauli hiyo ya Bashe, baadhi ya wafanyabiashara walisema pamoja na maelezo ya Waziri wa Kilimo juu ya umuhimu wa kuzingatia sheria, ubora na usalama wanaposafirisha mazao ya chakula, bado kuna vikwazo vingi vinavyohitaji kufanyiwa kazi ili malengo ya kuondoa vikwazo vya kibiashara yatimie.

Mwenyekiti wa Chama cha Wasafirishaji wa Mizigo Mkoa wa Arusha, Zainabu Athuman, alisema pamoja na fursa ya kufanya biashara za kimataifa, bado mifumo ya utoaji wa vibali, inahitaji kutazamwa upya ili kuziba mianya ya udanganyifu na kuondoa usumbufu.

Kuanzia Juni 7, mwaka huu, hakuna lori la mizigo lililoruhusiwa kuvuka mpaka kutokana na wafanyabiashara wa upande wa pili wa Kenya, nao kuzuia malori yaliyokuwa yanaingia Tanzania.

# Tril. 1.08/- zatolewa kuendesha miradi maendeleo

**Na Jenifer Gilla,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, amesema hadi Mei, mwaka huu, Sh. trilioni 1.08 sawa na asilimia 116, zimepelekwa kwenye mamlaka ya serikali za mitaa nchini kote kwa ajili ya kuendesha miradi ya maendeleo.

Kikwete aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Grace Tendega, kwa niaba ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Tendega katika swali hilo, alihoji kwa nini serikali haipeleki fedha za maendeleo katika halmashauri zote kwa wakati. Kikwete alisema fedha za maendeleo hutolewa katika mamlaka za serikali za mitaa baada ya halmashauri kuwasilisha maombi ya fedha za utekelezaji wa miradi husika.

Alisema miradi hutekelezwa na makandarasi na fedha hutolewa baada ya mkandarasi kutoa hati ya madai kwa kazi zilizofanyika kwa mujibu wa mikataba. "Serikali itaendelea kusimamia mikoa na halmashauri kuhakikisha maombi ya fedha za miradi ya maendeleo inaratibiwa na kuwasilishwa katika ngazi husika kwa wakati ili kuendelea na taratibu zingine za utekelezaji wa miradi.

"Kwa upande wa miradi inayotekelezwa kwa Force Account, fedha hutolewa kwa kuzingatia utayari wa Halmashauri kuanza utekelezaji wa mradi husika baada ya kuwasilisha maombi ya namna watakavyotekeleza mradi huo,"alisema. Katika swali la nyongeza, Mbunge huyo alihoji serikali ina mkakati gani wa kuwawezesha kifedha sekretarieti za mikoa ili zitekeleze wajibu wake ipasavyo.

"Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha halmashauri zote zinapata pesa kwa kiwango sawa kwa sababu zipo halmashauri ambazo zinapata pesa zaidi na nyingine pungufu,"alihoji.

Naibu Waziri huyo alisema Ofisi ya Rais, TAMISEMI itafuatilia fedha zote zinazopelekwa katika maeneo yote kwa mujibu wa kanuni inayotoa miongozo ya fedha inayotaka wahusika waombe fedha.

Pia alisema serikali haitoi pesa kwa upendeleo katika halmashauri kwa kuwa miradi inayotekelezwa ndio inayoongoza serikali kutoa fedha hizo.

# Wadau wajadili mfumo mpya mikopo kwa makundi maalum

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BAADA ya Rais Samia Suluhu Hassan, kusimamisha utoaji wa mikopo ya asilimia 10 kwa vijana, wanawake na wenye ulemavu, Jukwaa la Wadau wa Kilimo nchini (ANSAF) limeitisha mkutano wa wadau kukusanya maoni kuboresha usimamizi wa mfuko wa mikopo ya halmashauri ili iwe na tija kwa walengwa.

Hatua hiyo ya Rais, ilikuja mapema mwaka huu baada ya ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kubaini kuwa fedha za mikopo ambazo zimekuwa zikitolewa na halmashauri nchini, zaidi ya Sh. bilioni 88, zimetolewa kwa vikundi hewa na watu wasio na sifa.

Mkurugenzi Mtendaji wa ANSAF, Honest Mseri, alibainisha hayo jana jijini hapa, alipokuwa akizungumza kwenye mkutano wa wadau kukusanya maoni kuboresha usimamizi wa mfuko wa mikopo ya halmashauri kwa vikundi vya wanawake,vijana na watu wenye ulemavu.

Alisema wakati huu ambapo serikali ipo katika mchakato wa kuandaa mfumo ambao utasimamia utoaji wa mikopo hiyo ya asilimia 10, wameona kuna haja ya kuandaa mkutano huo ili kupata maoni ya wadau watakayoyawasilisha serikalini.

"Serikali ipo katika hatua za kuandaa mfumo ambao utatumika katika utoaji wa mikopo, hivyo tumeona kuwa na mkutano huu ambao unakutanisha wadau yakiwemo makundi ya vijana,wanawake na walemavu kutoka mikoa yote ili kupata maoni ambayo tutayawasilisha serikalini wayafanyie kazi.

"Siku zote sisi ANSAF, tunaamini kuwa maoni ya wahusika lazima yapewe kipaumbele katika kuboresha mfumo huu ndiyo maana hapa leo tunayo makundi yote yanayonufaika na mikopo hii ya asilimia kumi hivyo baada ya kuyapata maoni haya tutayapeleka TAMISEMI (Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa) ambao ndio wenye jukumu la kuratibu mfumo mpya," alisema.

Pia alisema alisema lengo la mkutano huo pia ni wadau kutoa maoni yao nini serikali ifanye ili kuboresha utoaji wa mikopo hiyo baada ya Rais kuisimamisha kutokana na ripoti ya CAG kuonyesha kuwa Sh. bilioni 88 zilizotolewa na halmashauri hazikusanyiki na hazikusanyiki.

"Baada ya ripoti ya CAG kutolewa, Mheshimiwa Rais alikasirika sana na kuagiza kuwa mikopo hii isimamishwe baada ya kuonekana kuwa kuna fedha nyingi ambazo zimetolewa katika vikundi hazija rejeshwa," alisema.

Pia alisema, jambo lingine ambalo lilionesha kasoro kwenye ripoti ya CAG ni mikopo kutolewa kwa vikundi hewa, watu kukopa katika halmashauri zaidi ya moja na mikopo kutolewa kwa wasiostahili.

"Katika mkutano wetu huu tutabishana kwa hoja na tutaondoka na mapendekezo mbalimbali na kuyapeleka serikalini na kuishauri namna bora ya kuendesha suala hili," alisema.

Ofisa Maendeleo ya Jamii kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Happy Hiza, alisema maoni ya wadau hao yatasaidia kuboresha utoaji wa mikopo ya asilimia kumi kwa vikundi mbalimbali ili kuleta tija.

"Wadau hapa watajadili mambo mbalimbali na kuboresha mfumo wa utoaji wa mikopo hii. Rais aliagiza mikopo hii ianze kutolewa kwa mfumo wa benki lakini tutajadili ili kuona namna gani wanufaika wanapata mikopo bila kuwa na usumbufu kama vile dhamana za benki ni kwa namna gani zitafika hadi maeneo ya vijijini ambako sisi tulikuwa tunawahudumia," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kwaheri msimu 2022 -23, tujipange kwa msimu ujao

**PAZIA** la Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2022-2023 lilifungwa rasmi jana Ijumaa kwa timu zote kushuka uwanjani, huku nyingine zikiaga ligi hiyo na nyingine kuingia kwenye kapu la Playoff.

Yanga kabla ya kufungwa kwa pazia hilo, tayari ilishatangazwa kuwa bingwa wa Ligi hiyo ikiwa ni mara ya 29 kwenye historia yao na sasa wanasubiri tu kucheza fainali ya kombe la FA dhidi ya Azam FC.

Kumalizika kwa ligi hiyo sasa kunafungua milango ya tathmini na kuangalia kwa pamoja na kujipanga kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu 2023-24 ambapo utaanza baadae Agosti mwaka huu.

Nipashe tunaamini kwamba, wakati huu ndio wa kufanya tathimini ya kweli kwa timu zote huku zikiangalia pale walipokosea na wapi walipopatia ili kuweza kuchukua hatua za kurekebisha makosa yao na kuwa bora zaidi kwa msimu ujao.

Tunaamini kwamba, kabla ya kuanza kwa msimu huu, kila timu ilikuwa na malengo yake iliyojiwekea, hivyo wakati huu ni muafaka sasa kuangalia makosa yao na wapi walikuwa na matatizo na kusababisha kushindwa kufikia malengo yao.

Timu ambazo zimeshindwa kufikia malengo yake tunaamini zitakaa chini pamoja na benchi la ufundi kuangalia mapungufu yaliyotokea na wapi wanapaswa kuparekebisha tayari kwa ajili ya msimu ujao.

Huu pia ni wakati wa viongozi na benchi la ufundi kuangalia aina ya wachezaji wanaowahitaji kwenye vikosi vyao ili kujiimarisha zaidi kwa msimu ujao ili waweze kufikia malengo yao.

Pia wale ambao wanawaona kuwa walikuwa mzigo kwenye timu pia ni wakati wa kuangalia namna ya kuwapa mkono wa kwaheri.

Pia wachezaji nao ni wakati wa kujitafakari wao wenyewe, wapi walifanya vizuri na wapi walikosea, ili kujiweka vizuri zaidi kwa ajili ya msimu ujao na pia ni wakati wa wengine kuachana na timu zao kwenda kutafuta malisho sehemu nyingine.

Kwa zile timu nne za kwanza kwenye Ligi hiyo, maana yake zitakuwa wawakilishi wa nchi kwenye mashindano ya kimataifa, hivyo wakati huu ni muhimu kwao kuangalia vikosi vyao wapi panapotakiwa kupaboresha.

Ikumbukwe kwamba, Simba na Yanga walikuwa kwenye mashindano ya kimataifa, Ligi ya mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Afrika.

Simba kwenye michuano hiyo waliishia kwenye hatua ya robo fainali, wakati Yanga walifika fainali ambapo walipoteza dhidi ya USM Alger ya Algeria.

Hivyo basi wakati huu ndio muafaka kwa timu hizo nne kutafuta na kuangalia aina ya wachezaji inaowahitaji kwenye vikosi vyao kwa ajili ya kufanya vizuri zaidi katika mashindano yajayo.


Iwapo timu itakuwa na kikosi imara kwenye Ligi Kuu, maana yake itaweza pia kutoa changamoto nzuri kwenye mashindano ya kimataifa, hivyo hii ni nafasi yao ya kufuta makosa.

Pia Bodi ya Ligi kwa upande wake huu nao ni wakati mzuri wa kuangalia wapi sheria na kanuni zilikinzana au zilileta utata hali iliyopelekea pengine kuleta taharuki yoyote.

Hivyo, Nipashe tunaona kwamba, Bodi ya Ligi sasa pia ndio wakati wao wa kutathimini sheria na kanuni zake ili kuiwezesha Ligi hiyo kuwa bora na yenye mafanikio makubwa zaidi.

Dosari zozote za sheria na kanuni zilizojitokeza kwenye Ligi hiyo msimu huu, zinatakiwa kutumika kama chachu ya kurekebisha makosa na kuziboresha ili kuwa bora na kuifanya ligi hii kuendelea kupaa barani Afrika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wachambuzi, mashabiki toeni maoni kanuni za Ligi

Na Adam Fungamwango

**BODI** ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), imefungua rasmi dirisha la kupokea maoni ya maboresho ya kanuni za Ligi Kuu, Championship na 'first league' kwa ajili ya maandalizi ya msimu wa 2023/24.

Ina maana mlango wa watu kutoa maoni umefunguliwa rasmi, na yeyote yule anaruhusiwa kwenda au kutuma kile ambacho anaona kinaweza kufaa kutengenezewa kanuni kwa ajili ya msimu ujao.

Taarifa hiyo imewataka wadau mbalimbali zikiwemo klabu za mpira wa miguu, mashabiki, wanahabari, vyama vya mpira wa miguu, wadhamini, taasisi za kiserikali na binafsi kuwasilisha mapendekezo yao kabla ya usiku wa Juni 30, 2023.

Hapa Bodi inatoa ufafanuzi wa nani anatakiwa kupeleka maoni, ili baadaye kusiwe na lawama kwa baadhi ya watu kuwa hawakushirikishwa, kuambiwa au kulaumu tu kile kilichoamualiwa kwa mujibu wa kanuni.

Bodi imekuwa na utaratibu wa kukusanya maoni kutoka kwa wadau wa mpira wa miguu hususan ligi hizo tatu ili kupata mawazo mapya ya namna ya kuendelea kuboresha uendeshaji na usimamizi wa ligi.

Wadau mbalimbali zikiwemo klabu za mpira wa miguu, mashabiki, wanahabari, vyama vya mpira wa miguu, wadhamini, taasisi za kiserikali na binafsi wanaombwa kutuma maoni yao kupitia anuani ya barua pepe Maoni@ligikuu.co.tz, kabla ya saa 5:59 usiku wa Juni 30, 2023.

Taarifa hii imejitosheleza kabisa, kwani imetaja wote wanaopaswa kutoa maoni yao, muda wa kumalizika na hata anuani ambayo maoni hao yanatakiwa yapelekwe.

Mbali na hilo, Bodi imewataka wadau pia kuwasilisha maoni yao kwa mkono kwenye ofisi za Bodi ya Ligi Kuu Tanzania zilizopo ghorofa ya 14 ya jengo ya NSSF (Mafao House), Ilala Boma, Dar es Salaam.

Maoni haya hutolewa kila msimu baada ya kumalizika kwa msimu wa mashindano yanayosimamiwa na Bodi hiyo ya Shirikisho la Soka Nchini (TFF).

Kila mwaka ligi inapokuwa inamalizika, bodi hutoa taarifa kuhitaji maoni mpya ili kufanya maboresho kwa ajili ya kanuni za Ligi Kuu, Championship na 'first league.'

Cha ajabu ni kwamba linapotokea tatizo lolote ambalo litahukumiwa hasa linalozihusu timu kubwa za Simba na Yanga na kuwa kinyume cha matakwa yao, mashabiki na hata wachambuzi wanakuja juu wakihoji udhaifu wa kanuni hizo.

Kazi ya kuziponda kanuni huanzia hapo na ushauri mwingi ambao kwa wakati huo hauna maana yoyote ile.

Huu sasa ndiyo wakati wa kutuma maoni, ili chochote kitakachoamuliwa kusiwe na wa kumlaumu mwenzake, kuanzia kamati, klabu, wanahabari, mpaka mashabiki.

Kwa wale ambao wanataka kanuni ya gari la wagonjwa ibadilike, basi huu ndiyo wakati wa kupeleka maoni yao.

Adhabu kwa timu zinazopita milango isiyotakiwa, dhana ya ushirikina, mgawanyo wa mapato ya mlangoni ambapo timu mwenyeji ndiye anayepata yote, nalo kama mtu anapinga aandike maoni.

Utitiri wa mechi za mchujo 'play off' Ligi Kuu, Championship na 'first league,' nazo zimekuwa zikilalamikiwa sana na wadau, sasa wana nafasi ya kwenda kushauri, kama ziondolewe au zipunguzwe.

Kanuni za wafungaji bora kama wakifungana, makipa kupewa 'clean sheets' hata wakicheza dakika tatu na kutoka na mengine mengi ambayo yanatakiwa kuunganishwa na kutengeneza kanuni ambazo hazitakuwa na malalamiko msimu ujao kwa sababu wadau wote wa soka watakuwa wamechangia kuzitengeneza.

# RC, wafanyabiashara wakutana ili kutatua kero zinazowakabili

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amekutana na wafanyabiashara wa mkoani hapa kujadili changamoto za biashara kwa ujumla na kuweka maazimio yenye tija katika kukuza masoko kwa kutumia fursa ndani na nje ya nchi.

Kikao hicho kilifanyika juzi katika Ukumbi wa jiji mkoani hapa na kuhudhuriwa na wafanyabiashara wakubwa, wakati na wadogo wakiwemo viongozi wa masoko, wamiliki wa shule, wamiliki wa nyumba za wageni, viongozi wa kampuni mbalimbali, wauza vipodozi na wafanyabiashara wa mbao.

Kikao hicho pia kilihudhuriwa na taasisi za serikali zikiwamo Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Wakala wa Afya na Usalama mahali pa kazi (OSHA), Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mamlaka ya Udhibiri Usafiri Ardhini (LATRA) na Wakala wa Usajili wa Leeni na Biashara (BRELA). Awali, wafanyabiashara walieleza changamoto mbalimbali zinazowakabili ndani ya masoko zikiwamo ulipishwaji wa kodi ya pango wakati si wamiliki wa nyumba, wingi wa kodi kwa wafanyabiashara, ubovu wa miundombinu ikiwamo barabara, upungufu katika ukaguzi wa risiti, mfumo wa ulipaji kodi usio rafiki na uzoaji wa taka na majitaka.

Baada ya kupokea kero hizo Senyamule alisema: "Sisi mkoa wa Dodoma tuna dhamira ya kuhakikisha wafanyabiashara wanakaa katika mazingira mazuri na tunajipanga kufanyia kazi changamoto na maazimio ili kuendelea kuboresha huduma katika nyanja zote."

Mkuu huyo wa mkoa alitoa rai kwa wafanyabiashara kuendelea kulipa kodi kwa serikali na kuwahakikisha uwapo wa mazingira rafiki ya biashara ikiwa ni utekelezaji wa agizo na maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan. Pia aliwataka kuunda umoja kulingana na biashara wanazofanya ili iwe rahisi kuratibu hoja zinazojitokeza na kuziwasilisha serikalini.

Katibu Tawala wa Mkoaa wa Dodoma, Ally Gugu, aliwapongeza wafanyabiashara kwa kujumuika katika kuwasilisha changamoto zilizo ndani ya masoko na kuweka kwa pamoja mikakati ya ufumbuzi na amewasisitiza kuhakikisha kazi hiyo inakuwa linakuwa endelevu.

"Serikali itahakikisha eneo letu la makao makuu ni sehemu sahihi na wezeshi kwa wafanyabiashara, hivyo lazima kuwa na mahali sahihi pa kufanya biashara eneo ambalo halitakuwa na changamoto ili biashara zishamiri na kupata faida kwa mmoja mmoja na serikali kwa ujumla," alisema.

Kikao hicho kiliazimia mambo ambayo yataboresha biashara ikiwamo halmashauri kuchukua hatua madhubuti kwa wanaomiliki vizimba na kutofanya biashara, kuundwa kwa timu itakayopitia sheria ya kodi ili kuunganisha serikali na sekta binafsi na kuundwa kwa kamati ya utatuzi wa changamoto za masoko kama ilivyokuwa kwa soko la Machinga.

Maazimio mengine ni pamoja na kuwepo kwa taasisi moja ya kukusanya tozo, jiji kukamilisha miundombinu kwenye baadhi ya masoko na kutoa elimu kwa umma hususan wafanyabiashara kuhusu matumizi ya mfumo wa TAUSI.

# Watoto 2,000 waondolewa kwenye ajira hatarishi

**Na Zuwena Shame**

ZAIDI ya watoto 2,600 mkoani Geita wameondolewa kwenye ajira hatarishi kwa kipindi cha miaka 10 kutipia mradi wa kutokomeza ajira mbaya kwa kundi hilo ulioendeshwa na shirika la Plan International nchini.

Mradi huo umetekelezwa kwa miaka 10 kwa ushirikiano wa Shirika la Plan International Tanzania, KIVULINI na Mpango wa Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi Tanzania (SEDIT) kwa ufadhili wa Ufaransa kupitia Shirika la Maendeleo la Ufaransa (FDA).

Hayo yalisemwa jijini Dar es Salaam jana na Kaimu Mkurugenzi wa Plan International Tanzania, Paul Lusato wakati wa kufunga mradi huo kwa awamu ya tatu.

Alisema ajira kwa watoto nchini bado ni changamoto kubwa kwani kutokana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (TNBS) inakadiriwa ni asilimia 21.9 ambapo pia inakadiriwa kuwa watoto milioni 4.9 kati ya umri wa miaka mitano hadi 17 wanajihusisha na shughuli za kiuchumi hasa kwenye kilimo, uvuvi, uchimbaji madini na kazi za ndani.

"Sisi tunaamini katika mabadiliko chanya na ushirikiano japo mdogo unaweza kuleta mafanikio makubwa, sisi na washirika wetu tumeweza kuokoa na kuwatoa watoto hawa katika ajira hatarishi na kuweza kuwapa haki yao ya msingi ya elimu na kuhakikisha kuwa wanabaki shuleni na kuwa na maisha bora ya baadaye," alisema Lusato.




Meneja Mwandamizi wa Mauzo Benki ya CRDB, Muhumuliza Buberwa (katikati), akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa kampeni ya "Timiza Ndoto yake na Junior Jumbo", jijini Dar es Salaam juzi, yenye lengo la kutoa elimu ya fedha kwa watoto na kuwahamasisha wazazi/walezi juu ya umuhimu wa kuwawekea watoto wao akiba ambapo benki ya CRDB imetenga Sh. milioni 15.4 kama zawadi ya ada kwa washindi wa kampeni hiyo ya kipindi cha mwezi mmoja. Kushoto ni Meneja Mauzo wa Benki hiyo, Amina Mawona na Meneja wa CRDB Tawi la Buza, Mary Joshua. **PICHA:**

# Serikali yaja na mikakati kuleta mageuzi ya kilimo

**Na Jenifer Gilla,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, amesema serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ya mageuzi ya kilimo nchini kwa lengo la kubadili kilimo kuwa cha biashara.

Amesema mikakati hiyo ni pamoja na kufanya kilimo kuwa na tija, uhimilivu na kinachoratibiwa na kusimamiwa na serikali na kushirikisha sekta binafsi ili kuwa na mifumo endelevu ya chakula na kilimo.

Aliyasema hayo jana bungeni wakati akijibu swali la Mbunge wa Singida Kaskazini, Abeid Ramadhani, aliyehoji kama kuna mkakati wa kufanya mageuzi ya kilimo nchini.

Mavunde, akijibu swali hilo alisema serikali kupitia bajeti ya mwaka 2023/24 inatekeleza vipaumbele na mikakati yenye lengo la kuongeza tija na uzalishaji, kuongeza ajira zenye staha na ushiriki wa vijana na wanawake kwenye kilimo, kuimarisha usalama wa chakula na lishe, kuimarisha upatikanaji wa masoko, mitaji na mauzo ya nje ya nchi na kuimarisha maendeleo ya ushirika.

Katika maswali ya nyongeza, mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani mahususi wa kuwapatia wakulima zana za kisasa hususani matrekta ili waachane na matumizi ya jembe la mkono.

Pia alitaka kufahamu serikali ina mpango gani mahsusi wa kufanya kilimo cha umwagiliaji kuwa ajenda ya kitaifa ili wakulima nchini waweze kulima mara mbili kwa mwaka kuondokana na kilimo cha kutegemea mvua.

Akijibu maswali hayo, Mavunde alisema serikali inashirikiana na Kituo cha zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC) na Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo (TEMDO) uzalishaji zana za kisasa za kilimo ili kufanya mageuzi katika zana hizo na wakulima walime kwa tija.

Alisema pia wanatarajia kuanzisha kituo cha mitambo katika ikolojia mbalimbali kikanda ili wakulima watumie fursa hiyo kukodi mitambo badala ya kwenda kukopa matrekta kwa gharama kubwa.

Aidha alisema kwa sasa mkakati mkubwa uliopo ni kuhakikisha skimu zote za umwagiliaji zinafanya kazi kwa kuweka vyanzo vya uhakika vya maji ili wananchi kuhudumia mashamba yao zaidi ya mara moja kwa mwaka.

# UN- HABITAT kufungua ofisi Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imetia saini hati ya makubaliano na Shirika la Umoja wa Mataifa la Makazi Duniani (UN- HABITAT), kuanzisha ofisi nchini, kuboresha makazi holela na kuwezesha ujenzi wa nyumba za gharama nafuu.

Makubaliano mengine ni kusaidia matumizi jadidifu ya nishati katika majengo, kupitia na kuandaa sera mpya ya miji, kuanzisha kituo cha taarifa ya makazi pamoja na kuboresha mifumo ya kitaasisi na uendelezaji miji midogo.

Makubaliano ya pande hizo mbili yalitiwa saini juzi jijini Nairobi, Kenya mbele ya mkutano wa UN-HABITAT na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika hilo, Maimunah Mohd Sharif.

Aidha, makubaliano yaliyofikiwa yatawezesha pia UN- HABITAT kuanzisha ofisi yake nchini Tanzania ili kurahisisha utekelezaji wa makubaliano hayo.

Akizungumza wakati wa utiaji saini makubaliano hayo, Dk. Mabula aliihakikishia UN-HABITAT kuwa Tanzania iko tayari kulipatia shirika hilo jengo la kuanzisha ofisi nchini.

Aidha, Dk. Mabula aliishukuru UN-HABITAT kwa misaada mbalimbali inayoipatia Tanzania sambamba na kupongeza uamuzi wa shirika hilo kuanzisha ofisi nchini.

"Naiomba UN-HABITAT kusaidia kuwajengea uwezo watanzania kwa kuwapa mafunzo na ajira za muda mfupi na mrefu ili kujenga uwezo," alisema Dk. Mabula.

Sharif alisema malengo endelevu ya makazi na nyumba yatafikiwa haraka kwa shirika lake kuwa na ofisi ya kudumu Tanzania na nchi zingine wanachama wa shirika hilo.

Alisema shirika lake kwa sasa linafanya maandalizi kabambe ya kuanzisha ofisi zake nchini Tanzania ili kuanza utekelezaji wa makubaliano hayo pamoja na kuondoa makazi holela ili kuwa na miji salama na iliyopangwa.

"Niihakikishie Tanzania kuwa UN-HABITAT iko tayari kutoa mafunzo na ajira za muda ili kuwajengea uwezo watanzania na kusaidia utekelezaji wa makubaliano yaliyofikiwa," alisema Sharif.

Kufunguliwa kwa ofisi za UN-HABITAT Tanzania, kutaharakisha maendeleo endelevu ya sekta ya makazi na nyumba na kutatoa ajira kwa Watanzania.

UN-HABITAT ni miongoni mwa mashirika ya Umoja wa Mataifa linaloshughulikia makazi ya watu na maendeleo endelevu ya miji na lilianzishwa mwaka 1977 kama matokeo ya mkutano wa kwanza wa Umoja wa Mataifa wa Makazi ya Watu na Maendeleo Endelevu ya Miji, uliofanyika Vancouver , Canada mwaka 1976.

Katika hatua nyingine, Tanzania na Kenya zimejadili kuboresha mahusiano katika sekta ya nyumba na makazi.

Waziri Mabula alisema serikali ya Tanzania iko makini kusimamia maendeleo ya sekta nyumba na makazi ili kukabiliana na ongezeko la idadi ya watu mijini linalofikia asilimia 4.8 kwa sasa.

"Moja ya juhudi za serikali ni utekelezaji wa mpango wa miaka 10 wa kurasimisha makazi holela ulioanza mwaka 2013," alisema.

Naye Waziri wa Kenya anayeshughulikia masuala ya Ardhi, Ujenzi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Zacharia Njeru, alisema nchi yake imeanzisha mpango kabambe wa ujenzi wa nyumba za gharama nafuu utakaowezesha ujenzi wa nyumba laki mbili kila mwaka.

Viongozi hao wawili walikubaliana kuunda kamati ya wataalamu wa pande zote mbili watakaosimamia utekelezaji wa makubaliano ya ushirikiano kati ya nchi hizo yaliyosainiwa mwaka 2021 jijini Dar es Salaam.




Watumishi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Joseph Mkonyi (anayebandika stika) na Neema Manyama wakishiriki zoezi la usajili kwa watoa huduma binafsi wa magari ya huduma za majitaka katika mabwawa ya Vingunguti, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Vitongoji 3,6101 kupatiwa umeme

**Jenifer Gilla,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, amesema serikali imekamilisha uhakiki wa vitongoji 36,101 visivyo na huduma ya umeme na kuandaa mradi kabambe wa kusambaza nishati hiyo katika vitongoji vyote unaojulikana kama 'Hamlet Electrification Project", vikiwamo vitongoji 262 vya wilaya ya Rorya.

Amesema mradi huo utagharamu Sh. trilioni 6.7 na unatarajiwa kukamilika hadi miaka mitano kulingana na upatikanaji wa fedha.

Byabato aliyasema hayo bungeni jana wakati akijibu swali la Mbunge wa Rorya, Jafari Chege, ambaye aliuliza serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha umeme unafika kwenye vitongoji vyote nchini.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) inatekeleza mradi wa kusambaza umeme vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili. Vijiji vyote nchini visivyokuwa na umeme hata kitongoji kimoja vitafikiwa na huduma hiyo.

# DAWASA yaanza usajili watoa huduma majitaka

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) imeanza kusajili watoa huduma binafsi na vibali vya uendeshaji wa magari yanayotoa huduma za usafi wa mazingira Dar es Salaam. Huduma ya usajili wa magari hayo itafanyika kwa muda wa wiki mbili eneo la Vingunguti jijini Dar es Salaam.

Akizungumza wakati wa kusajili magari hayo jana, Ofisa Biashara DAWASA, Mwajuma Hamza, alisema usajili huo ni endelevu na unafanyika kila mwaka kwa kushirikiana na watu binafsi ambao ni wamiliki wa magari ya majitaka.

Alisema huu ni waka wa sita tangu waanze utaratibu huo wa usajili ukiwa na madhumuni ya kupata takwimu sahihi za watoa huduma na kuhakikisha utoaji wa huduma za usafi wa mazingira zinaboreshwa kikamilifu kwenye mkoa wa Dar es Salaam.

"Leo tumeanza usajili na tunatarajia kuendesha usajili huu ndani ya wiki moja ili kuwatambua watoa huduma ambao huchukua majitaka kwa wananchi na kwenda kumwaga katika mabwawa yetu yaliyoko sehemu mbalimbali," alisema.

Aliongeza kuwa usajili wa magari utahusisha magari ambayo yana usajili wa zamani na magari mapya ambayo yameingia kwenye utoaji huduma hii ili waweze kutambuliwa na DAWASA katika uendeshaji wa huduma.

"Kwa magari yaliyosajiliwa awali, tunawaomba kufika kwa ajili ya kufanyiwa uhakiki ukiambatanisha na fomu inayoonyesha ujazo wa gari kutoka Wakala wa Vipimo nchini (WMA) na nakala yake," alisema Hamza.

Pamoja na hayo alisema baada ya muda wa usajili kuisha, yeyote atakayekutwa anatoa huduma ya kuchukua na kusafirisha majitaka katika eneo la huduma la DAWASA bila kibali hai cha uendeshaji atachukuliwa hatua kali za kisheria. Alisema magari yote yatakayopata vibali vya uendeshaji wa huduma yatabandikwa stika maalum za DAWASA.

Mrisho Mataula ambaye ni mmoja wa watoa huduma ya magari ya majitaka aliipongeza DAWASA kwa usajili huo kwani utawasaidia kwa kiasi kikubwa kutambulika na kuendesha shughuli zao kwa ufanisi mkubwa.

Alisema wamekuwa wakishirikiana na DAWASA kwenye maeneo ya shughuli zao hivyo kwa usajili huo unaoendelea wataondokana na usumbufu ambao umekuwa ukijitokeza mara kwa mara wanapokuwa kwenye shughuli zao za kila siku.

Aprili, mwaka huu, kampuni ya ujenzi ya Metito ya Misri, ilisaini mkataba wa kusanifu, kujenga na kuendesha mtambo mpya wa kuchakata majitaka katika eneo la Mbezi Beach, mkoani Dar es Salaam, Tanzania katika mradi huo unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya serikali na Benki ya Dunia (WB). Mradi huo unaotekelezwa na Serikali ya Tanzania kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), unatarajiwa kuchangia katika kuboresha usafi wa mazingira kwa kuwezesha majitaka kukusanywa na kutibiwa kikamilifu.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Kiula Kingu, alisema mtambo huo wa kisasa utakaojengwa eneo la Mbezi Beach, wilayani Kinondoni, utakuwa na uwezo wa kuchakata lita milioni 16 za majitaka kwa siku.



# Tatizo watoto wa kike kuacha shule lapungua

**Na Renatha Msungu**, DODOMA

TATIZO la wanafunzi wa kike kuacha shule katika baadhi ya shule za msingi wilayani Chemba mkoani Dodoma limefikia asilimia saba huku shule za sekondari ikifika asilimia tano.

Asilimia hizo zimejulikana baada ya utafiti uliofanywa hivi karibuni na Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/Met) katika mradi wa kuondoa vizuizi vya elimu kwa wasichana na wavulana unaotekelezwa na shirika lisilo la kiserikali la Woman Wake Up (WOWAP) katika shule mbalimbali za msingi na sekondari za wilaya ya Chemba.

Hayo yalisemwa na msimamizi wa mradi wa TEN/MET, Kenneth Nchimbi, wakati wa uzinduzi wa awamu ya pili ya mradi wa kuondoa vizuizi vya elimu kwa wasichana na wavulana uliolenga kupunguza utoro ili kuongeza idadi ya mahudhurio shuleni kwa watoto hao.

Nchimbi alisema awamu ya kwanza ya mradi huo ilikuwa na shule sita ambapo awamu ya pili imeongeza shule mbili zaidi hivyo kufikia shule nane ambazo pia zimeguswa katika utafiti huo.

Alizitaja shule za awamu ya kwanza na pili zilizo kwenye mradi huo lakini pia zimeguswa na utafiti huo ni Kelema Maziwani (msingi), Kwa Mtoro (sekondari), Soya (msingi), Mrijo (sekondari), Mrijo(msingi), na Soya (sekondari) Kelema Balai (msingi), na Chemba (sekondari).

Kwa mujibu wa Nchimbi, mradi huo pia umelenga kuboresha kiwango cha elimu kwa vijana wa rika hilo lakini pia kuongeza ufaulu kwa watoto pale wanapokuwa na mahudhurio mazuri shuleni.

"Bado kuna uwepo wa utoro kwa watoto wa kike katika shule za msingi na sekondari,hivyo uinduzi wa mradi huu wa pili utasaidia kutokomeza utoro mashuleni kabisa na kuongeza kiwango cha ufaulu," alisema Nchimbi.

Alisema utafiti wa tathmini ya mwisho ulionyesha kuwa mipango ya mradi ilifanikiwa kuchangia kufikia matokeo yanayotarajiwa,ikiwemo kupunguza kiwango cha wanafunzi wanaoacha shule hususani wasichana.

Kutokana na hali hiyo, alisema maeneo machache yanayohitaji juhudi zaidi ni pamoja na mafunzo ya stadi za maisha,kampeni za uelewa kwa wazazi, mikakati ya kudumisha klabu za shule ambazo zinatakiwa kuhusisha wasichana na wavulana.

# Katibu Mkuu ataka utatuzi migogoro kwa usuluhishi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Mkuu wizara ya Katiba na Sheria, Mary Makondo, amewataka mawakili wa serikali kutatua migogoro kwa njia ya majadiliano na usuluhishi ili kutengeneza mazingira mazuri yatakayowavutia wawekezaji.

Makondo, alisema hayo juzi wakati akifunga mafunzo ya siku tatu kwa Mawakili wa serikali pamoja na maadhimisho ya miaka mitano tangu kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Aidha, aliwataka Mawakili wa serikali kuhakikisha wanatumia mafunzo hayo kwenda kuongeza ufanisi katika taasisi zao na kusaidia kupungunza migogoro na mrundikano wa kesi mahakamani kwa njia ya majadiliono.

"Nchi ikiwa na migogoro, kesi na matukio yasiyofaa hakuna maendeleo hivyo serikali inatambua kazi kubwa mnayoifanya ila kaongezeni kasi ya utatuzi wa migogoro ili kuwavutia Wawekezaji.

"Wawekezaji wanataka sehemu ambako hakuna ubabaishaji kwanza wanaangalia usalama wa uwekezaji wao sasa basi kawadhihirishieni wawekezaji kuwa Tanzania ni eneo salama la kuwekeza kwa kuendesha majadiliano na kutengeneza

mazingira mazuri ya uwekezaji fanyeni hili kwa maslahi mapana ya nchi na watanzania kwa ujumla," alisema Makondo.

Aidha, alisema dunia kwa sasa imehamia kwenye dijitali hivyo ni lazima Mawakili nao wageukie huko kwa kutumia teknolojia na akili bandia kutatua migogoro na kupunguza mrundikano wa kesi mahakamani.

"Kwa sasa dunia imegeukia kwenye teknolojia sasa dijitali ndio inaongoza dunia hivyo hatuna budi na sisi kuelekea huku tutumie kurahisisha kazi na kutatua migogoro kwa wakati,"alisema

Pia, alizishukuru taasisi zote zilizowaruhusu Mawakili wa Serikali kuja kushiriki mafunzo hayo ambayo yamelenga kuwanoa ili waweze kuongeza ufanisi katika majukumu yao ya kila siku.

Wakili Mkuu wa Serikali Dk. Boniphace Luhende, aliishukuru wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana bega kwa bega na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na wadau wengine kuhakikisha mafunzo hayo yanafanyika.

Dk. Luhende alisema anaamini baada ya mawakili hao kunolewa kwa siku hizo tatu katika maeneo tofauti ikiwemo utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi na majadiliano itakwenda kupunguza mrundikano wa kesi mahakamani kwani utatuzi utafanyika kwa haraka kwa kuzingatia haki kwa pande zote mbili.

"Baada ya kunolewa kwa siku tatu naamini mmepata mambo mengi mapya sasa mkayatumie vyema kwa ajili ya ustawi wa taifa letu sitegemei tena kuona mrundikano wa kesi zisizoisha katengenezeni mazingira mazuri yatakayowavutia wawekezaji na mkasaidie eneo la manunuzi,"alisisitiza Dk.Luhende.



Mbunge wa Singida Kaskazini, Ramadhani Ighondo akichangia hoja, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Sheria kuhusu kazi walimu zaboreshwa

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

PROGRAMU ya Shule Bora kwa kushirikiana na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imefanya mapitio ya sheria zinazohusu kazi ya walimu ili ziwasaidie kuzielewa kwa urahisi tafsiri za sheria hizo.

Kwa mujibu wa ripoti ya Mei iliyotolewa na Programu ya Shule Bora na kusambazwa kwa vyombo vya habari jana, mchakato wa kuzipitia upya sheria hizo ulianzishwa baada ya kubainika kuwa sheria zilizopo zilikuwa ngumu kueleweka kwa baadhi ya walimu.

Taarifa ilibainisha kuwa Aprili, mwaka huu, TSC ilikamilisha kufanya mapitio ya sheria zilizorahisishwa na kuidhinisha zifanyiwe majaribio katika ngazi ya mikoa.

Kuhusu Umoja wa Walimu na Wazazi (UWaWa) taarifa ilisema umeonyesha mabadiliko chanya ya awali kwa kuimarishwa katika halmashauri. Walimu wakuu na wenyeviti wa kamati za shule wameendelea kutoa mafunzo katika ngazi ya shule. Aidha, katika mikoa mingi, UWaWa imekuwa ukizisaidia shule kutoa chakula kwa wanafunzi. Mfano katika Jiji la Dodoma, kati ya shule 93 za msingi, 68 zinatoa huduma ya chakula kwa wanafunzi wote kila siku wakati shule 38 zilizobaki zinatoa chakula kwa wanafunzi wa darasa la kwanza na madarasa ya mitihani (darasa la nne na la saba).

Ofisa Taaluma wa Jiji la Dodoma, Selina Shirati, katika ripoti hiyo alisema hivi sasa wanatarajia kupata matokeo bora ya elimu kufuatia ongezeko la ushiriki wa wazazi. "Kabla ya shule bora kuanzishwa, ni asilimia 40 tu ya shule zilikuwa zikitoa chakula kwa wanafunzi. Hivi sasa wazazi wanachangia vyakula na pesa kwa ajili ya kulisha watoto wao," alisema.

Shirati alisema wazazi pia washiriki katika kuwasaidia walimu kutengeneza zana za kufundishia hatua ambayo imeboresha matokeo ya ujifunzaji, usafi shuleni, na pia kuboresha masuala ya usalama na tahadhari.

Aidha, katika mkoa wa Simiyu, wajumbe wa UWaWa umehamasisha wazazi wa Shule ya Msingi Bariadi kuchangia kilo nne za mahindi na Sh. 2,000 kwa kila mtoto ili kukidhi mahitaji mengine ya kuni na sukari, pamoja na kulipa mishahara ya wapishi ambayo ni Sh. 50,000 kwa mwezi.

Program ya Shule Bora ambayo inafadhiliwa na serikali ya Uingereza kupitia mfuko wa UK Aid, inatekelezwa katika mikoa ya Singida, Dodoma, Simiyu, Tanga, Mara, Rukwa, Katavi, Pwani na Kigoma. Mambo yanayoboreshwa katika elimu ni kujifunza, kufundisha, jumuishi na kujenga mfumo.





## TAMWA yakoleza moto uwapo wa sera ya jinsia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, kimetaka uwapo wa sera ya jinsia katika vyombo vya habari ili kusaidia kuweka mazingira salama na kuondoa unyanyasaji.

Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema hayo jana katika mkutano wa maboresho ya sera ya jinsia kwa vyombo vya habari ambao umewakutanisha wadau mbalimbali. Mkutano huo ulifanyika Tunguu, wilaya ya Kati Unguja, katika ofisi za chama hicho.

Alisema hatua hiyo itasaidia kupunguza changamoto nyingi na kutoa fursa ya kuishi katika misingi imara ikiwamo kujitambua na kuheshimiana.

Alisema Zanzibar ni miongoni mwa nchi zilizojikita kuleta usawa wa kijinsia katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa, hivyo kuwapo kwa sera hiyo itakuwa chachu ya kufikia malengo ya kuwainua wanawake katika uongozi na kufikia asilimia 50 kwa 50.

Licha ya kuridhia mikataba mabalimbali ya kikanda na kimataifa ukiwamo wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) wa kuondosha aina zote za ubaguzi wa jinsia, alisema bado kuna maeneo yanahitaji kuwekewa mkazo zaidi ili kufanikisha malengo hayo.

Dk. Mzuri alisema kutokana na hali hiyo, vyombo vya habari vina jukumu la kuhakikisha kazi zao zinaleta usawa wa kijinsia na kuondosha aina zote za ubaguzi na kulinda haki za binadamu.

Akiwasilisha mambo muhimu yaliyomo kwenye sera ya jinsia ya vyombo vya habari Mkufunzi kutoka Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Idara ya Mawasiliano na Taaluma za Habari, Imane Duwe, alisema uwapo wa sera hiyo utasaidia kutengeneza mazingira salama na bora ili kuondosha mwanya wa aina zote za unyanyasaji.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuwa na utaratibu thabiti wa kuripoti masuala yote ya jinsia na kuviwezesha vyombo vya Habari kuweka usawa wa kuripoti masuala mbalimbali yanayohusu jinsia zote.

Pia alisema sera hiyo itasaidia kutoa miongozo na kutanua wigo katika kupaza sauti za wanawake kupitia shughuli mbalimbali wanazozifanya ikiwemo uzalishaji mali na shughuli nyengine ili kuondosha mawazo mgando ya kumkandamiza mwanamke.

Akisisitiza maboresho ya sera hiyo, Shifaa Said Hassan kutoka Baraza la Habari Tanzania alivitaka vyombo vya habari kuanzisha sera ya jinsia na kuzifanyia kazi ipasavyo ili kuweka mazingira salama ya taasisi hizo na wafanyakazi wake.

# Ujenzi viwanda wawa kichocheo kwa wakulima wa mwani Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imewataka wakulima wanawake kuchangamkia fursa ya kilimo cha mwani kutokana na ujenzi wa viwanda viwili ambavyo vitaongeza thamani ya usarifu na uchakataji wa bidhaa hiyo na hatimaye kuingia katika soko la kimataifa duniani.

Hayo yalisemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi (BLW) na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum, wakati akijibu hoja za wajumbe kuhusu mikakati ya SMZ katika kuwawezesha wajasirimali wanawake kuingia katika uchumi wa bluu.

Waziri huyo alisema kilimo cha Mwani kwa asilimia 90 kinalimwa na wanawake katika maeneo ya pembezoni mwa fukwe, hivyo ni fursa nzuri kujikita katika kilimo hicho kutokana na ujio wa viwanda viwili vya kuchakata zao hilo.

Alisema serikali imeanza kujenga kiwanda cha kusarifu na kuongeza thamani ya mwani Chamanangwe kisiwani Pemba huku akiwataka wakulima wajipange kukidhi mahitaji ya kiwanda hicho.

Pia alisema kiwanda kingine kinatarajiwa kujengwa Dunga, wilaya yaKati Unguja ambacho kitakidhi mahitaji ya soko kwa upande wa wilaya hiyo yenye uzalishaji mkubwa wa mwani.

Alisema ujenzi wa viwanda hivyo ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020- 2025 inayolenga kuhakikisha wakulima wa mwani ambao kwa asilimia 90 ni wanawake, wanapiga hatua kubwa na kujikomboa kiuchumi.

"Mheshimiwa Spika, tunakwenda kujenga viwanda viwili vya kusarifu na kuongeza thamani ya zao la mwani. Viwanda hivyo ni mkombozi kwa mwanamke katika kupambana na hali ngumu ya uchumi hasa wale wanaoishi ukanda wa pwani," alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi ya BLW, Sabiha Filfil Thani, alisema soko la mwani limeingia katika mabadiliko makubwa na mwani aina ya Ulva ndiyo iliyotawala katika soko la bidhaa hiyo huku ikiwa na kipato kikubwa.

Aliwataka wakulima wa mwani kuongeza uzalishaji kutoka tani 1,200 hadi 4,200 za aina ya hiyo na kwamba tayari kampuni kutoka Uingereza imeanza kununua kutoka kwa wakulima.

Waziri wa Maendeleo ya Biashara na Viwanda, Omar Said Shaaban, alisema wameanza kutoa elimu kwa wakulima kuhusu kilimo cha mwani aina ya Ulva pamoja na matunzo yake ili kuhakikisha unaingia katika soko la bidhaa hiyo.

Alisema aina hiyo ya mwani inahitaji matunzo mazuri ikiwamo kukaushwa vizuri na kuondoa takataka zote pamoja na kuepuka mazingira ya unyevunyevu.

Shaaban alitoa ufafanuzi huo baada ya Mwakilishi wa Chambani Bahati Khamis Kombo, alipoilalamikia wizara kushindwa kununua mwani aina ya Ulva ambao umelimwa na wakulima wa jimbo lake bila ya kufahamu sababu za msingi.

WOaziri Shaaban alisema mwani aina ya Ulva ni mgeni katika soko la Zanzibar kwa hiyo wakati wanunuzi wakiununua, walitoa kasoro mbalimbali ikiwamo unyevunyevu mwingi, hivyo kusababisha harufu.



Wafanyakazi katika Kiwanda cha uzalishaji wa mbegu bora zikiwemo za alizeti, mahindi na ufuta cha Highland Seed Growers Ltd, wakifungasha kwenye mifuko mbegu za mahindi zilizoboreshwa tayari kwenda kwa mkulima kwa ajili ya matumizi, jijini Mbeya juzi. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# Mkataba ujenzi barabara watiwa saini

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) imetiliana saini na kampuni ya URKUN ya Uturuki kwa ajili ya ujenzi wa barabara ambazo zinaendelea kujengwa.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Khadija Khamis Rajab, alitia saini kwa niaba ya serikali huku ORKUN Group ikiwakilishwa na Mkurugenzi wake, Cumhur Baris Kochan.


Akizungumza baada utiani saini, Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed, aliwataka wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa miradi inayotekelezwa ili kufikia lengo la kuziunganisha barabara zote visiwani hapa.

Waziri alisema dhamira ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ni kuziunganisha barabara zote mijini na vijijini ili kuimarisha uchumi na hali za kimaisha za wananchi.

Kuhusu ujenzi wa barabara za mjini, Dk. Khalid alisema kuna haja ya kufanyiwa tena matengenezo kwa sababu zimejengwa muda mrefu tangu miaka ya 1970 hali inayosababisha wakati wa mvua kuchimbika.

Pia alisema barabara zinazotarajiwa kujengwa kupitia mradi huo ni za Jumbi-Tunguu (kilomita nane), Bungi (kilomita nane) na Charawe, Ukongoroni-Bwejuu (kilomita 23).

Mradi wa ujenzi uliotiwa saniwa utagharimu zaidi ya Dola za Kimarekeani milioni 27.



**NICK MINAJ**

UKURASA 14

Nipashe MWANGA WA JAMII

BT BURUDANI TELE

JUMAMOSI JUNI 10, 2023

# LONA: AMBER LULU ANAPENDA KUPIGWA



ALIYEKUWA mpenzi wa msanii na video queens maarufu nchini Amber Lulu, Lona ameibuka na kuweka wazi kwa nini mahusiano yao yamedumu kwa kipindi kifupi tu, akidai mwenzake huyo anapendwa sana kupigwa.

Lona, ambaye ni mkali ya kucheza video za wasanii mbalimbali wa kike amesema mapenzi yake na Amber Lulu yalidumu kwa miezi mitano tu, lakini akaona 'bora yaishe' kwani akiendelea naye anaweza kwenda jela.

"Alikuwa mpenzi wangu lakini kwa sasa tumeachana, mapenzi yetu yamedumu kama miezi mitano hivi, sababu ni mimi, nadhani mimi ndiyo nimeshindwa, nimemuacha afanye michongo yake na mimi nifanye yangu.

Tatizo Amber Lulu ni mwanamke ambaye anapenda sana ugomvi, ni wale wanawake ambao yeye mpaka apigwe ndiyo anajiona yuko sawa. Anapenda sana kupigwa, nikaona bora nikae pembeni maana naweza kwenda Segerea, mimi kukimbizana na polisi mimi siwezi." Akasema.

Akasema inawezekana kabisa hata stori za mumewe wa zamani walizokuwa wanasikia kuwa amepigwa na baadhi ya watu kumtetea kwenye mitandao ya kijamii, alikuwa yupo sahihi "Mimi nafikiri hivyo." Alisema.

Akisimualia baadhi ya visa vyake alisema kwanza ana wivu ambao unasababisha agombane hata na baadhi ya rafiki zake.

"Yalinikuta mimi, kwa sababu mimi ni mpole sana, ikifika mpaka imekuwa hivyo ni noma sana."

Akasimuliwa baadhi ya visa ambavyo vimesababisha hali hiyo.

"Mara nyingi tukiwa klabu au tumetoka, basi ni mwanamke ambaye anakuwa na wivu sana, halafu wivu wenyewe unaenda tofauti. Mmekaa hata mahali hataki ugeuke, hata uende chooni. Kuna wakati anagombana hata na marafiki zake," alisema.

Lona alikanusha tuhuma zinazodai alikuwa 'akilelewa' na Amber Lulu, badala yake akadai yeye ndiye alikuwa analipa kodi ya nyumba.

"Mimi siyo wa kulelewa, hapana alikuwa kwake na mimi kwangu Sinza, lakini baada ya kukutana ikabidi kila mtu atoke kwake tuchue nyumba ya kuishi pamoja Mbezi Juu mimi nikalipa kodi, baada ya kuachana yeye sasa anaishi Salasala, mimi kwa sasa nimeshatoka Sinza ninaishi Kijitonyama," alisema Lina.

Kabla ya kuwa na Lona, msanii huyo alikuwa na mwanaume mwingine anaitwa, Botion.

BASI SAWA

## Golden TZ yuko 'Lonely'



MSANII wa muziki wa kizazi kipya, Golden TZ, ametoa singo ya wimbo kwa mfumo wa video uitwao 'Lonely.

Msanii huyo ni moja kati ya vijana waliokuzwa na kulelewa na Tanzania House of Talent (THT) na amekuwa kwenye tasnia ya muziki kwa muda mrefu, ingawa kwa miaka ya karibuni alikuwa kimya.

Ngoma yake imeshaanza kukonga mioyo ya mashabiki wa bongo fleva kutokana na umahiri wake.

Ameshawahi kutoa ngoma mbalimbali huko nyuma kama 'Wako', 'Tawire' aliyomshirikisha Jay Melody, 'Siwezi', 'Kaza Roho'. 'Unayumba', 'Baadaye', 'Yala' na nyingine nyingi.

## Swagg kufanya 'kolabo' na Nyoshi

Salmin Swagg, msanii wa bongo fleva amesema anafikiria kufanya 'kolabo' moja kali na mwanamuziki wa dansi maarufu nchini, Nyoshi El Saadat.

Msanii huyo amesema anatarajia kufanya hivyo ili iwe kumbukumbu ya kufanya kazi ya mkongwe huyo kwenye tasnia ya muziki dansi, lakini pia ikitajwa kuwa ni mkwewe.

Swagg, amekiri kuwa na mahusiano ya Blandina ambaye ni binti ya Nyoshi, lakini hakutaka kuelezea sana hilo kwa madai hapendi sana mambo yake kuwa hadharani.

"Blandina yupo nyumbani, ni mpenzi wangu, ni binti wa mwanamuziki hiyo, ila siwezi kuweka sana vitu vyangu nje, unajua ukishakuwa maarufu kila unachokifanya lazima kitakwenda hadharani hata kama wewe hukutana kufanya hivyo," alisema.

Kuhusu 'kolabo' na mkwewe amesema anatarajia kufanya hivyo.





# TUNDA MAN, MATONYA BIFU LAO HADHARANI

Miaka kadhaa nyuma, mashabiki wa bongo fleva watakumbuka kuwa wasanii Tunda Man na Matonya walikuwa na bifu, lakini hakuna hata mmoja aliyekuwa anajua lilitokana na nini.

Hatimaye Tunda Man wiki hii amefichua sababu hasa ya ugomvi wao baada ya miaka mingi kupita.

Tunda Man amebainisha kuwa Matonya alimkasirikia baada ya kutoboa siri kuwa yeye ndiye aliyemuandikia moja ya nyimbo zake.

"Mpaka leo ugomvi wangu na Matonya ni kusema tu kwamba nimemuandikia wimbo, unajua zamani ukisema eti umemuandikia mtu wimbo,inakuwa kama dhambi hivi, mtu anakasirika," anasema Tunda Man na kuongeza.

"Halafu mpaka sasa wakongwe wengi wa muziki huu wa bongo fleva hasa wale wa zamani wanaamini hivyo, na wanashindwa kurudi kwenye gemu kwa sababu tu hawaamini kuandikiwa. Unajua ubongo wangu haupo kwenye kizazi hiki cha sasa, unajua kila kizazi kina maneno yake, hawa wa sasa nitawaandikia maneno gani mpaka wakanielewa? Kumpa heshima yake mtu aliyekuandikia siyo kwamba wewe huwezi kuandika. Unajua elimu na akili ni vitu viwili tofauti, unaweza ukawa na elimu usiwe na akili na unaweza ukawa na akili usiwe na elimu, lakini ni bora uwe na akili. Kwa sababu ukiwa na akili, unaweza kuandikiwa wimbo ukamtaja aliyekuandikia wewe umeuimba, sasa hapo umepungukiwa nini? Kila mtu atanufaika, mtu akitaka shoo atanipigia mimi na akitaka kuandikiwa wimbo atampigia aliyeniandikia, wote mtapata pesa," Tunda Man akafichua.



# Walter Chilambo amkumbuka Nay wa Mitego

Mwimbaji wa zamani wa bongo fleva ambaye kwa sasa anaimba nyimbo za injili, Walter Chilambo amesema anamkumbuka sana msanii Nay wa Mitego na kukubali kazi zake, lakini pia ndiye aliyempa changamoto na kumfanya awe hapo alipo.

Walter ambaye ni mshindi wa Bongo Star Search mwaka 2012, amesema kwa muda mrefu sasa hajaonana na Nay wa Mitego kutokana na kwamba harakati zao zipo tofauti kwani yeye sasa anaimba injili, lakini anamkubali kwa ngoma zake, na hata maneno ambayo aliwahi kumwambia kipindi fulani yalimuongezea umakini kwenye muziki na maisha kwa ujumla.

Nay alishawahi kumchana Walter miaka ya nyuma, kitu ambacho wengi walitarajia kuwa wanaweza kuwa hawana uhusiano mzuri.

"Na siyo Nay tu, marafiki wangu wengi sana sijaonana nao kwa sababu wao wapo kwenye bongo fleva na mimi injili, hatuonani, kama tumetofautiana harakati fulani kwa hiyo si rahisi kukaa pamoja. Unaona leo umeniuliza, ilinibusti, ilinifanya nifahamike zaidi na hata kama kuna sehemu nilikosea ilinifanya nijitafakari," alisema.

# DK. CHAMELEONE ALIVYOWATESA WABONGO

**Na Adam Fungamwango**

ANAITWA Dk. Jose Chameleone, huku jina lake halisi likiwa ni Joseph Mayanja. Ni mzaliwa na nchini Uganda. Huyu ni msanii maarufu sana si Afrika Mashariki na Kati tu, bali Afrika nzima kwa sasa.

Kitu kinachomtofautisha na wasanii wengine wa Uganda ni baadhi ya nyimbo zake kuimbwa kwa lugha ya kiswahili. Tena kiswahili fasaha.

Ndiyo maana Chameleone ndiyo msanii ambaye anatambuliwa zaidi na kipenzi cha mashabiki wa muziki wa Tanzania.

Amejizolea mashabiki wengi nchini kutokana na si tu kuimba kiswahili, lakini hata ngoma zake anazotoa zimekuwa bora na kuwapagawisha watu.

Mara kwa mara amekuwa akitoa ngoma za kiswahili ambazo zimekuwa zikitamba sana kwenye redio na televisheni za Tanzania.

Hizi ni baadhi ya ngoma ambazo pamoja na kuwa ni Mganda, lakini zimemfanya awe maarufu zaidi Tanzania.

**Shida za Dunia**

Hii ni moja ya ngoma za mwanzo kabisa zilizomtambulisha Dk. Chameleone. Ilitoka mwanzoni mwa miaka ya 2000 na wengi walidhani kuwa ni msanii kutoka Tanzania kwa jinsi alivyoimba wimbo huu.

Ni wimbo unaozungumzia mtu mmoja akilia shida baada ya kupata matatizo kufukuzwa kazi na mkewe kumtoroka, lakini rafiki yake anamwambia aache kulia kwani ni shida tu za dunia na Mwenyezi Mungu anamjaribia, ipo siku mambo yatakaa sawa.

**Jamila**

Ni ngoma ambayo ilizidi kumuweka msanii huyo Mganda kwenye mioyo ya Watanzania. Ngoma hii ilimzungumzia demu mmoja ambaye aliachwa na mpenzi wake na akawa ana majonzi makubwa na kububujikwa na machozi. Ili kupata ushauri nasaha alikwenda kwa Chameleone ambaye naye hakuwa na kazi nyingine ila kumbembeleza.

**Badilisha**



Katikati ya miaka ya 2000, Dk. Chameleone alikuja kivingine kwa kutoa ngoma yake kali aliyoiita 'Badilisha'.

Ngoma hii ilizidi kumpa heshima nchini Tanzania, kiasi cha kuitwa mara kwa mara kwa ajili ya kutunukiwa tuzo kwenye mashindano ya miziki ya Kitanzania na ile ya kiswahili pia.

**Valuvalu**

Ni ngoma iliyopendwa na Wabongo wengi kuelekea mwishoni mwa miaka ya 2000. Ni wimbo wa mapenzi ambao Chameleone alikuwa akimwambia mpenzi wake kuwa anampenda awe wake na aachane wa watu valuvalu ambao hawapendi kuona mapenzi yao yanaendelea.

Ngoma hii ilizidi kumuweka msanii huyo mioyoni mwa Wabongo ambao hadi wapende ngoma yako uwe umefanya kazi kweli kweli.

**Tubonge**

Ngoma hii ndiyo ilifunga kazi kweli kweli. 'Tubonge' ni ngoma ambayo iko zaidi kwenye uelekeo wa wimbo wa 'gospel', yaani wimbo wa Injili. Lakini kwa jinsi ulivyopigwa ni kama bongo fleva tu, ila maneno yake ni ya Injili, hivyo baada ya kutoka ulikonga nyoyo za mashabiki wote wa muziki wa bongo fleva na Injili pia. Ukawa unapigwa kotekote, ukienda kwenye miziki ya kidunia upo na miziki ya kumuimbia Bwana unapigwa pia na watu wanaserebuka kama kawaida.

FILAMU

# Binti Yatima: Msukule hadi mke

**Na Adam Fungamwango**

FILAMU ya 'Binti Yatima', inazungumzia juu ya binti mmoja yatima, lakini aliyekuwa na karama ya kuagua na kutengeneza dawa mbalimbali.

Baada ya mama yake kufariki, na kuwa yatima, anachukuliwa na kaka yake Rasta binamu na kuletwa mjini, lakini kazi yake ikiwa ni moja tu, kumfanya kuwa na uwezo wa kipesa.

Rasta anamuweka ndani, anamtesa na kumfanyia kila aina ya unyanyasaji. Anamtumia kununua shamba na nyumba kwa bei rahisi. Ni kwamba binti huyo ambaye jina lake ni Victoria akifanya dawa zake, kaka yake ananunua kitu kwa bei ambayo anaitaka yeye.

Victoria hakuruhusiwa kutoka ndani, badala yake alikuwa amefungiwa ndani na kufanywa kama msukule.

Filamu hii imechezwa na Denis Kalamka, Ally Matika, Jamal Khamis, Victoria Mwigoni, Steven Mwakitenga na wengineo wengi.

Upande wa pili kuna kijana anazurura mitaani aliokota makopo, Jina lake Wembe. Kuna siku alikosa chakula kabisa, akabaki amekaa chini ya mti. Akapita dada mmoja akiwa na vitumbua, akamuomba. Dada alimuonea huruma, akampa.

Siku ya pili Wembe katika pitapita yake kiu ikamshika, akaenda kwenye nyumba moja kuomba maji. Ghafla akakutana na msichana yule yule aliyempa vitumbua siku chache nyuma. Akapewa maji ya kunywa. Dada huyo anaitwa Shanaiza.

Rasta anamlazimisha dada yake amtengenezee dawa ya mapenzi kwani jana yake alikutana na msichana akamtongoza lakini akamkataa. Victoria akafanya kama alivyoagizwa. Msichana anaingia laini. Si mwingine ni Shanaiza. Siku moja akiwa na mpenzi wake Rasta anakutana na Wembe. Shanaiza anambembeleza Rasta ampe chumba kimoja nyumbani kwake kwa sababu hana pa kukaa na ni rafiki yake sana. Rasta anatekeleza hilo. Moja ya masharti anayopewa ni kutofungua chumba kimoja. Ndicho alichomfungia dada yake binamu. Siku moja Wembe alifungua na alichokutana nacho alishangaa. Akakutana na msichana ambaye angekuwa mrembo sana kama angekuwa na matunzo. Akamhadithia yote yaliyomkuta. Wakapanga mpango, wakatoroka.

Huku nyuma dawa zikaisha nguvu, Victoria hayupo, Rasta akachanganyikiwa. Shanaiza akamtema Rasta kwa sababu mapenzi yalikuwa ya dawa. Victoria akafanya vitu vyake, Wembe akaanza kupata pesa, wakaoana.





# Nicki Minaj achia albamu mpya

MWANAMAMA nyota mwimbaji maarufu duniani Nicki Minaj ametoa albamu yake ya kwanza baada ya takriban miaka mitano.

Mara ya mwisho kutoa albam ilikuwa ni 2018, huku miaka iliyobaki alikuwa akitoa singo tu, lakini safari hii akaona akonge nyoyo ya mashabiki wake kwa kuja na LP.

Mwimbaji huyo mwenye vituko raia wa Trinidad and Tobago, jina lake halisi likiwa Onika Tanya Maraj-Petty, ametoa albamu hiyo ambayo inasemekana itakuwa kali kuliko zote ambazo ameshawahi huzitoa.

Aliitangaza mwenyewe kwenye mtandao wake wa twitter na kupokelewa vema na mashabiki, ambapo maoni zaidi ya 100,000 yalitolewa kuonyesha kufurahishwa na tukio hilo.

Albamu ya mwisho ya Queen Minaj mwaka 2018, aliwashirikisha mastaa kibao kama Eminem, Foxy Brown, Future na wengineo.



## Mzazi mwenzake Jessie J huyu hapa

Hatimaye mwanamuziki mwimbaji, raia wa Uingereza, Jessie J amemuonyesha mzazi mwenzake ambaye ni mcheza mpira wa kikapu, Chanan Safir Colman.

Mwezi Mei, mwimbaji hiyo alijifungua mtoto wake wa kiume, lakini hakumtaja baba yake, kitu ambacho kikazua minong'ono kwa mashabiki wake na wa muziki kwa ujumla.

Jessie J, ambaye jina lake kamili ni Jessica Ellen Cornish, alimtambulisha baba watoto wake kwenye mtandao wake wa Instagram wiki hii, akizima kiu ya wengi japo mwenyewe alisema hapendi sana mambo yake binafsi kuweka au kuwekwa kwenye mitandao

"Siwezi kuweka siri na kila kitu," aliandika na kuweka picha na video kadhaa na mwanaume huyo aliye mtaja kama baba wa mtoto wake Colman.

## Mtoto wa P Diddy adakwa kautwika njwiii

Mtoto wa rapa wa Kimarekani, P Diddy, Justin Combs amedakwa na polisi huko Los Angeles, California kwa kosa la kuendesha gari huku akiwa amelewa.

Kijana huyo mwenye miaka 29, alidakwa wiki hii majira ya asubuhi maeneo ya Beverly Hills, baada ya afisa wa polisi kuona gari likipita kwenye taa nyekundu bila kusimama, ndipo afisa mmoja akatoa ishara ya kusimamisha, aliposimama walimkuta Combs ndiye anayeendesha gari.

Kwa mujibu wa jarida la TMZ, gari lake lilipekuliwa, maafande wakajidhirisha kuwa kulikuwa na sababu za kutosha za kumkamata kwa tuhuma kwamba alikuwa yuko nywii, ameutwika.

"Maafisa walisimamisha na walimwona dereva akiwa amekunywa pombe au dawa za kulevya," ilisema Idara ya Polisi ya Los Angeles iliambia Fox News. "





## 2 Chainz aomboleza kifo cha mbwa wake

RAPA wa Kimarekani, 2 Chainz ameandika ujumbe mzito baada ya kifo cha mbwa wake wiki hii.

Mwanamuziki huyo wa kufokafoka alithibitisha kifo cha mbwa wake, Trappy baada ya kukaa naye kwa zaidi ya miaka minane.

Kwenye mtandao wake wa Instagram amesema anatafakari kwa uchungu maisha aliyokuwa anaishi na mbwa huyo kama rafiki mkubwa.

"Hata nikisema hili moyo wangu unaumia nimekuwa na Trappy kwa miaka tisa, tumesafiri na kuzunguka duniani kote na hayupo tena nami, iliniumiza najiskia kama mtu amekufa, nampenda mbwa wangu alikuwa na akili sana, lakini sasa amelala." Akaandika kwa uchungu.

Akasema anakumbuka vitu vingi na kumbukumbu za Trappy na hataki kuamini kama hatosikia akikoroma tena.

## Erick Omondi atarajiwa kuitwa baba

Mchekeshaji maarufu kutoka nchini Kenya, Erick Omondi ameweka wazi kuwa anatarajia kuwa baba kwa mara ya kwanza baada ya miaka 40.

Omondi, kupitia ukurasa wake wa instagram ameshea picha akiwa na mpenzi wake Lynn akionyesha kuwa ni mjamzito na akasindikiza kwa kuandika ujumbe akimshukuru Mungu, akisema anatarajia kupata mtoto wake wa kwanza kwenye maisha yake, akimshukuru pia mpenzi wake kwa kumpa zawadi hiyo.

Omondi mwenye miaka 41, anatarajia kupata mtoto wa kwanza kwenye maisha yake, ndiyo maana amekuwa hafichi furaha yake kwa kutarajia kumpata 'first born' wake.







Kaimu Meneja wa Bandari ya Tanga, Peter Milanzi (kulia), akipokea kikombe cha ushindi wa jumla wa maonyesho ya biashara na utalii kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba juzi, baada ya kuwa mfadhili mkuu wa maonyesho hayo. **PICHA: BONIFACE GIDEON.**

# Mradi wa afya waokoa watoto wachanga 100, wajawazito 25

**Na Allan Isack,** BABATI

WATAALAMU wa afya mkoa wa Manyara, wameokoa maisha ya zaidi ya watoto wachanga 100 na wajawazito 25 waliokuwa hatarini kupoteza maisha kwa kukosa huduma bora za kitaalamu.

Wataalamu hao, wameokoa maisha ya watu hao baada ya kuanza utakelezaji wa mradi wa Kitita cha Uzazi Salama, ulioanzishwa kwa lengo la kuboresha huduma za afya hasa kupunguza vifo kwa wajawazito na watoto.

Akizungumza jana alipotembelea Hospitali ya Wilaya ya Babati kukagua jengo la mama na mtoto, Mkurugenzi wa Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe kutoka Ofisi ya Rais,Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Ntuli Kapologwe, alisema mradi huo umekuwa msaada kwa wanawake na watoto na umeleta matokeo chanya.

"Tulichofurahishwa tangu mradi huu,umeanza kutekelezwa katika mkoa wa Manyara, umesaidia kuokoa maisha ya zaidi ya watoto wachanga 120 na kinamama 25. Jambo hili limetufurahisha sana tumeona ni muda mwafaka kupeleka mradi huu katika mikoa mingine," alisema.

Alisema kutokana na mafanikio hayo kuleta matokeo chanya, wameweka utaratibu wa kuupeleka mradi wa kitita katika mikoa mingine minne ya Tanzania Bara.

Mratibu wa Mpango wa Mradi wa Kitita cha Uzazi Salama Mkoa wa Manyara, Beatrice Githiri, alisema wamekuwa wakitoa vifaa na mafunzo kwa wauguzi ili kuokoa maisha ya wajawazito na watoto.

Alisema mradi umesaidia kuboresha huduma kwa wateja na umepunguza vifo kwa kuwa awali hakukuwapo vifaa vya kutosha na utaalamu wa kutoa huduma hasa kutoa hewa kwa watoto ipasavyo baada ya kuzaliwa.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Babati, Dk. Renatha Herman, alisema mradi uko katika vituo sita na unajihusisha kuokoa vifo vya kinamama na watoto wachanga kabla na baada ya kujifungua.

"Tangu kuanzishwa kwa mradi huu mwaka 2021, wanawake 7,421 wamepatiwa huduma za afya na watoto waliosaidiwa kupumua ni 127 kwa kuwa bila kuwapo kwa ujuzi na vifaa bora na vya kisasa wangepoteza maisha kwa kukosa msaada huo. Pia vifo vya kinamama na watoto vimepungua kwa asilimia kubwa,"

## Wizara yasisitiza chanjo kwa watoto

**Na Jaliwason Jasson,** ARUSHA

WIZARA ya Afya imewaagiza wazazi nchini kuhakikisha watoto chini ya miaka mitano wanapatiwa chanjo bila kukwepa ili kuwaepusha kupata madhara ya kiafya ikiwamo surua.

Kadhalika, wazazi wanaohamahama wameagizwa kutoa taarifa kwa wenyeviti wa vijiji ili wasaidiwe wanakokwenda kuhamia.

Agizo hilo lilitolewa jana na Meneja wa Mpango wa Taifa wa Chanjo, Dk. Florian Tinuga, wakati akitoa semina kwa waandishi wa Kanda ya Kaskazini iliyofanyika jijini hapa.

"Mzazi asikae na mtoto bila kupata chanjo na tusikubali mtoto kukaa ndani bila kupata chanjo. Tutumie vituo vyetu na njia ya mkoba watoto wapate chanjo," alisema.

Dk. Tinuga alisema watoto wakiachwa bila kuchanjwa na wakija kuchanjwa kipindi cha mlipuko ni gharama kubwa kwa taifa.

Meneja huyo alisema sababu za wazazi kutopeleka watoto kupata chanjo ni jamii kuhama hama na mila potofu.

"Msihame na watoto ambao hawajapata chanjo au akihamia mahali inatakiwa kutoa taarifa kwa wenyeviti ili awaunganishe na zahanati mnakohamia,"alisema huku akiuhakikishia umma kuwa hakuna chanjo inayoingizwa serikalini kama ina tatizo.

"Chanjo kuingizwa nchini,inapitiwa na kamati ya wanasayansi ambayo inamshauri Waziri wa Afya juu ya chanjo hiyo," alisema.

Pia alisema wameendelea kufanya vizuri na nchi imefika asilimia 90 kwa utoaji wa chanjo kwa watoto.

Mtaalamu huyo alisema mwaka 2019 mpaka 2022 waliachwa watoto chini ya miaka mitano na wengi hawakukamilisha dozi.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Dk. Silvia Mamkwe, alisema katika vitu vinawaumiza akinamama ni kansa ya shingo ya kizazi.

Dk. Mamkwe alisema ugonjwa huo, ukigundulika mapema unatibika na alieleza kuwa kipimo kinachofanyika ni kipimo cha kawaida.

Ofisa Mpango wa Taifa wa Chanjo katika Wizara ya Afya, Lotalis

# RAS akumbusha uwajibikaji viongozi ushirika

**Na Tumaini Mafie**,ARUSHA

KATIBU Tawala Mkoa wa Arusha, Missaile Musa, amewataka viongozi wa vyama vya ushirika kuwajibika kwa wanachama na kuwakumbusha kuwa wanapaswa kulaumiwa wanapokosa na wala si serikali.

Mussa alitoa kauli hiyo jana wakati akifunga mafunzo ya viongozi wapya wa vyama vya ushirika wanaosimamia wakulima wa mboga na matunda kutoka halamshauri tatu za mkoa wa Arusha yaliyofanyika kwa siku tatu.

Musa alisema serikali imekuwa ikitupiwa lawama vyama vya ushirika vinaposhindwa kusimamia sheria na viongozi wa vyama hivyo. Alisema wanaopaswa kutupiwa lawama hizo ni viongozi hao.

"Mara nyingi vyama hivi vinaposhindwa kusimamia wajibu, lawama zinatupwa serikalini lakini ukweli ni kwamba viongozi wanaongoza vyama hivi ndio wanaopaswa kulaumiwa, hivyo nawaagiza mkafanye kazi kwa kufuata miongozo na taratibu stahiki ili kuleta tija katika vyama vya ushirika," alisema.

Katibu Tawala alitaka pia kuaajiri watendaji wataalamu wa kilimo cha matunda na mboga kwa lengo la kufikia mafanikio yaliyokusudiwa katika sekta ya kilimo na kuinua uchumi wa nchi.

Mratibu wa Mafunzo hayo, Ndimolo Laizer, ambaye ni Ofisa Ushirika kutoka Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, alisema mafunzo hayo yamewakutanisha wajumbe wa bodi za vyama vya ushirika vya msingi vinavyosimamia mazao ya bustani (mboga na matunda).

"Mafunzo haya yamelenga kujenga uelewa kwa viongozi wa vyama vya ushirika vya msingi kabla ya kuanza majukumu ya kuhudumia wanachama wanaowasimamia,namna ya kufanya kazi kwa kushirikiana na mamlaka nyingine na zisizokuwa za kiserikali," alisema Laizer.

Mshiriki wa mafunzo hayo, John Mangi, akizungumza niaba ya wenzake, aliiomba serikali kuangalia suala la lumbesa kwa umakini kwa wakulima kwa kuwa limekuwa likiwaumiza.

"Tunaomba serikali ifanyie kazi suala la lumbesa kwani linatuumiza sisi wakulima kwa kuwa limedumu kwa miaka mingi, hivyo tunaomba iliangalie. Jambo lingine ni ugawaji wa mbolea za ruzuku kwamba idadi ya mbolea iendane na aina ya mazao husika na ipatikane kwa wakati," alisema Mangi.

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Michezo ya UMISSETA ilivyozalisha vinara wa soka nchini ngazi ya Taifa

**Na Adam Fungamwango**

NI Wiki hii kitaifa, kumefanyika tukio la kuzindua michezo ya shuleni, UMITASHUMTA kwa ngazi za shule za msingi, na UMISSETA kwa sekondari, baada ya kuonekana kusuasua na wakati fulani kufikia hatua ya kusimamishwa, ikatoweka kabisa.

Ikirejewa historia yake, ni aina ya michezo ambayo ina mchango mkubwa ya kukuza burudani hiyo kitaifa kwa ngazi ya klabu, timu za mikoa na taifa, hata kipaji cha mchezaji mmoja mmoja.

Itakumbukwa hasa kwenye miaka ya 1970 hadi 1980, uundwaji wa timu za mikoa na usajili wa mchezaji mmoja mmoja katika klabu nyingi za soka nchini, kwa nafasi ya pekee UMISSETA imetoa mchango mkubwa.




Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Philip Mpango akipuliza filimbi kuashiria Ufunguzi rasmi wa Mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA yanayofanyika Juni 6 mwaka huu, Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi Mkoani Tabora.

Sura hiyo ndiyo inatawala hata kwenye mpira wa kikapu na netiboli, tegemeo kubwa la wachezaji walitokea kwenye nguzo hiyo, mfano hai jijini Dar es Salaam, timu maarufu za mpira wa kikapu kama Pazi ikiwa na nyota mmoja wapo, Hassan Mtwangi maarufu kama 'Tiger', alikuwa mwanafunzi wa shule ya sekondari Tambaza, huku mpinzani wake mkuu uwanjani, Adam Kasidi Hunter, ametoka sekondari ya Kinondoni Muslim.

Hata majina hayo yametokana upinzani wao uwanjani, mmoja ni mnyama aina ya chui na mwingine ni mwindaji, bashasha zilizonogesha mno mpira wa kikapu. Wapinzani hao walipokutana kwenye mechi za UMISSETA, baina ya Tambaza na Kinondoni Muslim kunawaka moto, hali kadhalika hao hao wakikutana kwenye klabu zao hasimu, Vijana na Pazi panachimbika.

Mbali na hao, kwenye shule zingine nako kulitikisa kwa namna yake kukiibua nyota wa UMISSETA wanaojitokeza kwenye timu zingine za mpira wa kikapu, mfano hai ni mwanafunzi wa sekondari ya Ndanda ya Masasi Mtwara, Stephen Patrick Mbundi, aliyetokea sekondari ya Kibiti, Pwani, naye alitikisa mno uwanjani, akiwa mchezaji wa timu ngumu kwenye michuano ya wakati huo Benki Kuu (ambayo baadaye ilimuajiri).




Hii ni stempu ya Shirika la Posta na Simu Tanzania wakati huo miaka ya 1980, ikiwa na picha ya nahodha wa timu ya soka, Taifa Stars, Jellah Mtagwa ambaye chimbuko lake ni UMISSETA akitokea Sekondari ya Mzumbe, Morogoro.



Moja kati ya mechi za Mashindano ya Shule za Sekondari, UMISSETA ambayo miaka ya nyuma ilitoa wachezaji wengi kwenda klabu kubwa zikiwemo Simba na Yanga, pamoja na timu ya taifa, Taifa Stars. **PICHA ZOTE : MAKTABA**

Kilichojiri kwenye mpira wa kikapu, ndicho kilichotawala kwenye mpira wa pete, maarufu kama netiboli, katika zama zake ikiwa kileleni, ikitamba nchini.

Kulikuwa na timu nyingi kama vile Bora, Jeshi Stars, Magereza, Bandari, Akiba, Nyuki, msingi wa wachezaji wake wengi ni zao la UMISSETA.

Sasa mtikisiko usio na mfano kwa michezo hiyo ulishuhudiwa kwenye soka, ambayo hakuna namna ya kutenganisha kung'ara kwake nchini miaka hiyo na mavuno ya usajili kutoka UMISSETA.

Kwa sasa klabu nyingi za Ligi Kuu zinasajili wachezaji kutoka nje ya nchi na kwenye klabu mbalimbali za Ligi Kuu, lakini wakati huo, ilikuwa kinyume chake, wachezaji wanavunwa hata katika ngazi ya mkoa, lakini huibuka kuwa vinara wa kutikisa soka la kitaifa na kimataifa.

Klabu kubwa hata za Simba na Yanga zilikuwa zinakwenda kuvuna wachezaji kutoka shule za sekondari na hata msingi.

Kuna wakati usajili wa klabu ya Simba ukang'arishwa na kikosi 11 uwanjani zao la UMISSETA, wengi wakitoka shule za Dar es Salaam, kama George Kulagwa, Abass Kuka, Daniel Mwalusamba, na kinara wa shule ya sekondari Forodhani, Nico Njohole, hilo ndilo likashuhudiwa hata kwenye usajili wa baadaye, zao la UMISSETA kwenye timu hiyo, akiwa ameshahitimu kwenye shule ya sekondari Kibasila, akashuhudiwa mlindamlango maarufu, Moses Mkandawile.

Ndiyo hali iliyotawala hata kwa watani wao wa jadi, Yanga, wakati fulani mwanzoni mwa miaka ya 1990, wakamsajili katika hali ya kumgombania, winga wa UMISSETA aliyetamba mkoani Shinyanga, Edibily Lunyamila, akitua Dar kuvaa jezi ya njano na kijani, baada ya kutoroshwa kwa ndege, mkataba ukifanyika angani, kabla ya hapo nyuma walikuwa wameshasajili wachezaji, mmojawapo kinara wa soka nchini, Ahmed Amasha kutoka Sekondari jijini Dar es Salaam.

Simulizi kama hizo, zinaangukia hata katika umaarufu wa klabu ya Pamba ya Mwanza iliyotoa wachezaji wengi ngazi ya Taifa, waliokwenda pia kujiunga na klabu za Simba na Yanga, kwa kiasi kikubwa nao, waliibukia shule za sekondari, hususan za mkoani Kagera. Hapo huwezi kuwa mbali na majina kama Fumo Felician aliyetikisa kwa mashuti makali na 'guu' lake la kushoto.

Katika orodha hiyo, pia ni vigumu kusahau majina kama George Masatu na Nkama Ntale.

Mkoani Tanga, hususan klabu ya Coastal Union, wao ilikuwa kama vile wana mkataba na shule pia mamlaka ya UMISSETA, kwani nyota wake wengi walitokea huko na wakawa zawadi kubwa hata kwa timu ya taifa, Taifa Stars, hapo wanakumbukwa mshambuliaji namba 10, Hussein Mwakuruzo akitokea sekondari ya Jumuiya Tanga, baada ya kujenga uwezo mkubwa akisoma shule ya msingi, Kibasila, Dar es Salaam.

Sehemu mojawapo ya kilele cha mafanikio, ni pale ilipoanzishwa klabu ya Pan African, ikimeguka kutoka Yanga katikati ya miaka ya 1970, wakamsajili mlinzi wa kati Jellah Mtagwa, mwanafunzi wa shule ya sekondari Mzumbe, Morogoro ambaye hata kushirikishwa kwake uwanjani kwenye mechi za mwanzo ilikuwa mgogoro, lakini aliendelea kung'ara kutikisa hadi timu ya taifa kuanzia zama ana miaka miwili sekondari na kuna wakati kufikia, picha yake kuwekwa kwenye stempu ya nchi, akiwa nahodha wa Taifa Stars.

Baadhi yao, kwa sababu za kimasomo, na kihistoria waliibukia ngazi ya Chuo Kikuu, msingi wa soka lao ukiwa ni Sekondari, hao ni Leodger Tenga mwanafunzi wa Uhandisi Mitambo, na mwenzake mchumi, Lawrence Mwalusako, wote kutoka Chuo Kikuu cha Dar es salaam, wote waliwahi kuichezea Yanga, Tenga akikipiga Pan African kwa muda mrefu. Pia walidumu timu ya Taifa.

Kwa maana hiyo kinachofanyika hivi sasa, kufufua michezo, UMITASHUMTA na UMISSETA, una tafsiri kubwa kwa maendeleo ya michezo kitaifa.

# Trump anakabiliwa na mashtaka saba

**NEW YORK,** MAREKANI

RAIS wa zamani wa Marekani, Donald Trump ameshtakiwa kwa kushughulikia nyaraka za siri baada ya kuondoka Ikulu ya White House.

Trump mwenye umri wa miaka 76 anakabiliwa na mashtaka saba ikiwa ni pamoja na kuhifadhi faili za siri zilizoainishwa bila kibali, vyombo vya habari vya Marekani viliripoti.

Hili ni shitaka la pili dhidi ya Trump na shtaka la kwanza kabisa la kutoka upande wa serikali kwa rais wa zamani.

Trump amekuwa akifanya kampeni ya kurudi Ikulu katika uchaguzi ujao wa mwaka 2024.

Katika chapisho kwenye mtandao wa Truth Social, Trump alisema hakuwa na hatia na ametakiwa kufika katika mahakama mjini Miami Jumanne alasiri, ambapo atakamatwa na kusikiliza mashtaka dhidi yake.

"Sikuwahi kufikiria kuwa jambo kama hilo linaweza kumpata rais wa zamani wa Marekani," aliandika.

Aliongeza: "Kwa hakika hii ni siku ya giza kwa nchi ya Marekani, lakini kwa pamoja tutaifanya Marekani kuwa Kuu tena!"

Wakili wa Trump, Jim Trusty aliambia shirika la habari la CNN kuwa rais huyo alikuwa amepokea maelezo ya mashtaka katika hati ya wito.

Alisema ni pamoja na kula njama, taarifa za uongo, kuzuia haki, na kuhifadhi nyaraka za siri kinyume cha sheria chini ya sheria ya Ujasusi.

Idara ya Haki (DOJ) ilikataa kutoa maoni na hati ya mashtaka haijatolewa hadharani.

Hati ya mashitaka ni hati inayoweka wazi maelezo ya mashtaka dhidi ya mtu, kuhakikisha kuwa ana taarifa ya makosa ya jinai yanayodaiwa.

Wakati huo huo, maofisa wa ujasusi wa siri watakutana na wasimamizi wa sheria ili kupanga safari ya Trump hadi mahakama ya Miami katika siku zijazo.

Mwendesha mashtaka maalum, Jack Smith amekuwa akizingatia ushahidi katika kesi ya hati tangu alipoteuliwa kuisimamia na Mwanasheria Mkuu, Merrick Garland Novemba.

Mwaka jana, nyumba ya kifahari yake Trump iliyopo Florida ilipekuliwa na hati 11,000 zilinaswa, zikiwemo takribani 100 zilizowekwa alama kama zilizoainishwa.

Kulikuwa na ripoti wiki jana kwamba waendesha mashtaka walipata rekodi ya sauti ya Trump ambapo alikiri kuhifadhi hati za siri baada ya kuondoka Ikulu.

Ni kinyume cha sheria za Marekani kwa maofisa wa serikali - ikiwa ni pamoja na rais - kuondoka au kuweka hati zilizoainishwa katika eneo lisiloidhinishwa.

Wataalamu wa sheria walisema kufunguliwa mashtaka hakutazuia uwezo wa Trump kuwania tena kiti cha urais.

"Anaweza kushtakiwa mara kadhaa na haitazuia uwezo wake wa kugombea nafasi," alisema David Super, Profesa katika Kituo cha Sheria cha Chuo Kikuu cha Georgetown.

Super alibainisha kuwa Trump anaweza kuendelea kuwania wadhifa huo hata kama atapatikana na hatia katika kesi hiyo ya stakabadhi.




Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken katika picha ya pamoja wakati wa mkutano wa baraza la mawaziri wa ushirikiano wa nchi za Ghuba (GCC), mjini Riyadh nchini Saudi Arabia baada ya mazungumzo na Waziri wa Mambo ya Nje wa Saudi Arabia Mwanamfalme Faisal bin Farhan na kiongozi wa taifa hilo Mwanamfalme Mohammed bin Salman. **PICHA:BBC**

# Sudan yamkataa mjumbe wa Umoja wa Mataifa

**KARTHOUM,** SUDAN

SERIKALI ya Sudan imemtangaza mjumbe wa Umoja wa Mataifa nchini humo, Volker Perthes, kuwa "mtu asiyekubalika", kumaanisha kuwa haitambui tena nafasi yake.

"Serikali ya Jamhuri ya Sudan imemjulisha Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kwamba imemtangaza Volker Perthes... mtu asiyekubalika kuanzia leo," Wizara ya Mambo ya Nje ilisema katika taarifa yake.

Perthes alikuwa jijini Addis Ababa siku ya Alhamisi kwa ajili ya msururu wa mazungumzo ya kidiplomasia, kwa mujibu wa mtandao wa Twitter wa ujumbe wa Umoja wa Mataifa.

Mkuu wa majeshi ya Sudan - na kiongozi mkuu wa Sudan - Jenerali Abdel Fattah al-Burhan, hivi karibuni alimshutumu Perthes kwa kuchochea mzozo wa nchi hiyo.

Kabla ya kuanza kwa mzozo kati ya jeshi na wapinzani wake wa kijeshi, Rapid Support Forces, mjumbe wa Umoja wa Mataifa nchini Sudan alikuwa akilengwa na maandamano ya kulaani madai ya kuingiliwa na mataifa ya kigeni.

# Urusi yashutumiwa kushambulia waliohamishwa

**KHERSON,** UKRAINE

UKRAINE imeishutumu Urusi kwa kushambulia maeneo ya kuhamisha watu walioathiriwa na uvunjifu wa bwawa la Kakhovka, baada ya mtu mmoja kuuawa huko Kherson.

Ofisi ya mwendesha mashtaka wa Kherson ilisema watu wengine wawili pia walijeruhiwa, huku wizara ya mambo ya ndani ikisema kuwa wengine nane walijeruhiwa kwa kushambuliwa kwa makombora katika uwanja wa Korabelna.

Mashambulizi hayo yametokea wakati Rais Volodymyr Zelensky alipotembelea mji huo, ambapo alikutana na wenyeji walioathiriwa na mafuriko.

Watu 2,000 wamehamishwa kutoka eneo hilo, gavana wa Kherson alisema.

Akizungumza katika taarifa ya video iliyotumwa kwenye mtandao wa Telegram, Oleksandr Prokudin alisema "uhamishaji kutoka maeneo ya mafuriko unaendelea" licha ya "hatari kubwa na makombora ya mara kwa mara ya Urusi".

Ukraine inasema mafuriko yameathiri eneo la karibu kilomita za mraba 600 na maelfu ya watu wameachwa bila maji ya kunywa.

Jeshi la Ukraine limetumia ndege zisizo na rubani kudondosha chupa za maji na chakula kwa baadhi ya wakazi.

# Rubi ya Msumbiji yauzwa kwa Dola Mil 35

**NEW YORK,** MAREKANI

JIWE la madini aina ya Rubi ambalo ni kubwa zaidi kuwahi kupigwa mnada limeuzwa jijini New York nchini Marekani kwa rekodi ya chini ya dola Mil 35.

Jiwe hilo lenye karati 55.22, liligunduliwa mwaka jana katika mgodi mmoja nchini Msumbiji.

Kabla ya kukatwa ilikuwa na karati 101 na limepewa jina la "Estrela de Fura" kwa Kireno likimaanisha "Nyota ya Fura." Jina hilo linarejelea kampuni iliyochimba jiwe hilo.

Rubi zilizopigwa rangi ya zaidi ya karati tano ni nadra sana kupatikana duniani.

Kampuni ya Sotheby's, ambao walipiga mnada jiwe hilo, iliielezea kama kito cha "mara moja katika maisha".

Mnada huo huo pia ulishuhudia jumla ya rekodi iliyopatikana kwa almasi ya waridi.

Jiwe la karati 10.5 kutoka Botswana inayoelezewa kama jiwe la kupendeza la zambarau linauzwa kwa chini ya dola Mil 35.

# MATUKIO KATIKA PICHA



Akinamama wakijitolea kukarabati barabara ya nusu kilomita kwa kutumia majembe katika mtaa wa Mabanda ya Papa, wilayani Muheza, mkoani Tanga jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**




Wakili kutoka Abc Attorneys, Winnie Kamandakamu (katikati), akikabidhi zawadi kwa Mwanafunzi bora wa sheria ya mali miliki, Angelina Anney (kushoto), katika maadhimisho ya Siku ya Taaluma 2023 ya Shule ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**




Meneja Mauzo wa Airtel mkoa wa Kagera, Aaron Ntangalo (kulia), akikabidhi zawadi ya friji kwa Mkazi wa kata ya Bwanjai, Wilaya ya Missenyi, mkoani Kagera, Jasson Kataboro (wa pili kulia), baada ya kuibuka mshindi wa promosheni ya "Upige Mwingi", mjini Bukoba mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**




Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (wapili kushoto), akizungumza na wadau wa madini ya Tanzanite wa mji mdogo wa Mirerani, Wilayani Simanjiro, jana. **PICHA: GIFT THADEY**




Mkuu wa mkoa wa Arusha, John Mongela akizungumza katika mkutano wa jukwaa la maendeleo ya ushirika mkoa wa Arusha jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**



Mkulima Thomas Mkola (kushoto)' akiwa na wakili wake, Penina Ernest wakielekea katika chumba cha Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam juzi, kusikiliza kesi aliyoifungua ya kuwashtaki mawaziri na wizara zilizotajwa katika Ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusishwa na ubadhirifu wa fedha za umma. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# HADITHI

MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumba moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake. Ilitokea kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, viungo vya mwili wa binadamu vilianguka. Majirani wa kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Akinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.

## MAITI KWENYE KIROBA-12

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

Hakutaka kujisumbua na lolote lile, akili yake ilimtuma kuwa akijua ratiba za safari za mtu huyo ndipo anaweza kujua kama anaweza kuwa msaada na kuanza naye upelelezi, au kutafuta kitu kingine, au kubadili aina ya upelelezi kwa ajili ya kusaka muuaji wa mwanamama Tessy.

Aliachana na kompyuta baada ya kutuma email na sasa hakutaka kujishughulisha na kitu chochote, akaanza kusoma magazeti, taarifa moja iliyoandikwa kwenye magazeti matatu tofauti ndiyo iliyomvutia zaidi.

Akakenua meno, na kutojulikana kama ni tabasamu au mshangao. Alirudia tena kusoma sasa mwanzo hadi mwisho. Vichwa vya habari hiyo viliandikwa hivi 'Muuaji wa Tessy bado kizungumkuti.' Lingine likaandikwa 'Polisi wataka uvumilivu mauaji ya Tessy', la tatu liliandikwa 'Bado muuaji anasawa.'

Wakati akisoma habari yenyewe ndani, ilionekana kabisa wananchi wamekata tamaa ya kupatikana kwa muuaji, kwani ni miezi sita sasa inaonekana hakuna chochote kinachoendelea, huku muuaji huyo aliyeua na kukatakata viungo vya marehemu kama nyama ya buchani, akiendelea kula na kunywa uraiani.

******************************

Siku mbili baadaye akiwa ofisini kwake aliletewa magazeti, vichwa vya habari vilionyesha kuwa watu watano wamekamatwa wakishukiwa na mauaji ya 'Tessy.'


Kwake Eddy haikuwa taarifa nzuri. Siyo kwamba hakutaka muuaji asipatikane, lakini hakutaka wakamatwe watu wanaoshukiwa, badala yake muuaji halisi. Yeye kwa muda mfupi tu ambao amelifuatilia hili swala hakuamini kama hao waliokamatwa ndiyo wenyewe.

Alinyanyua mkono wa simu ya mkononi, akampigia Inspekta Frank.

"Upo Mkuu?" Akasalimia kwa kuuliza.

"Nipo, niambie, nadhani kazi inaendelea."

"Ni kweli kazi inaendelea, nimeshaianza, ila kama tulivyosema, au nilivyokwambia kwenye kikao kilichopita kuwa sina sababu sana ya kuweka wazi. Nitaweka wazi pale nitakapoona inafaa."




**"Okay nimekuelewa." Alijibu Maria kwa sauti ya chini kidogo, lakini ya msisitizo.**

"Haina shida, nimefarijika tu kuniambia kuwa umeshaianza."

"Ni kweli na wala usipate tabu, ila nina kitu kimoja naomba nikushauri."

""Enhee, niambie Eddy."

"Hao watu niliosikia mmewakamata, naomba waachieni."

"Kwa nini? Nimeletewa taarifa kuwa wanaweza kuwa ndiyo wenyewe." Eddy alicheka, halafu akamjibu.

"Mimi ni Mtanzania, tena mzalendo, huwa nachukia sana ninapoona kuna Watanzania wenzangu wanakatwa kwa makosa ambao ni ya kushukiwa, au kusingiziwa. Kwa muda mfupi tu ambao nimeanza kufanya upelelezi, tena siyo wa kutembea, hao mliowakamata siyo wenyewe."

Sauti ya Eddy ilipenya vizuri masikioni kwa Inspekta Frank, ikionyesha ni kama mtu mwenye uhakika na anachokisema. Mpelelezi maarufu kama huyo akiongea hivyo, yeye ni nani hadi abishe?

"Sasa tunafanyaje?" Akauliza Inspekta.

"Naomba waachieni, hao hawawezi kuwa wauaji. Tayari mimi nimeshaanza kuelekea kwenye njia ambayo muuaji ameifuata. Nadhani mambo yakienda vizuri tunaweza kumpata au kuwapata, ni kuvuta subira kidogo tu."

"Sawa nimekuelewa, labda wewe ungeshauri nini?"

"Kwa hili, ushauri wangu ni kwamba kama unaweza wasimamishe watu wako kushughulikia hili suala. Niachieni mimi tu."

"Sawa mimi nimekuelewa, lakini labda hebu niambie sababu ili nikiwaambia hata mabosi wangu wanielewe."

"Ni hivi, Inspekta, mtakapokuwa mnawakamata watu tofauti tofauti hata nyinyi wenyewe mtaonekana kama hamjui mnachokifanya, Mtaonekana mnababahatisha. Haiwezekani mkawa mliwakamata waokota makopo na watupa taka mkawaachia, halafu tena mmewakamata tena mmewakamata watu watano, sasa kama mimi nikifanikiwa kumpata muuaji halisi, inakuwaje hapo? Mnaonekana vipi? Hata wananchi hawatokuwa tena na imani na nyinyi. Afande mimi nafanya kazi kwa niaba yenu na tayari mabosi zangu wameshapata barua rasmi kutoka kwenu na kunipa ruhusa ya kufanya hili, nadhani sasa ungewaambia vijana wako wapumzike, mpaka baadaye tena, maana tunaweza kuchanganyana." Akashauri.

"Vizuri nimekuelewa, nitafanya hivyo." Inspekta Frank alikubali.

****************************

Alipomaliza kuongea na afande huyo alichukua simu yake ya mkononi, akabonyeza vitufe na kuiweka sikioni.

"Niambie mtoto wewe umeshatoka ofisini?"

"Ndiyo si uliniambia nitoke."

"Ni kweli, sikutaka tuongeee maneno haya uko ofisini, vipi umeshamaliza kazi?"

"Nimemaliza, nipo kwenye gari yangu narudi nyumbani sasa."

"Enhee kazi yangu umeniambia umeifanya, inasemaje?"

"Nimeifanya na nitakutumia kesho kwenye email yako, lakini kwa kifupi mtu uliyoniambia nifuatilie safari zake ni kwamba, mara zote safari zake ni za kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma. Kwa uchunguzi wangu mfupi tu ni kwamba huyu ni mtumishi wa umma, yaani ni mfanyakazi wa serikali. Inaonekana kwamba ana safari nyingi tu za Dar na Dodoma, lakini nyingine hatumii ndege, anatumia magari ya kawaida tu ya serikali, ila mara hizi ambazo ninakutumia kwenye mtandao anatumia usafiri wa ndege."

"Du, nadhani umeanza kunipita hata mimi mwenye kazi yangu." Eddy alitania. Maria akaangua kicheko.

"Umeona eee, inabidi uwe uniajiri niwe nakusaidia." Akajibu na sasa ikawa zamu ya Eddy kucheka.

"Ni mara moja tu ambayo safari yake haikuwa ya Dar Dodoma au kutoka Dodoma kuja Dar."

"Alaa, alikwenda wapi?"

"Inaonekana alitoka Mwanza kuja Dar tu na kesho yake, akatoka Dar kwenda Dodoma."

"Katika safari hizo zote, ipo siku ambayo alitoka Dodoma kuja Dar, halafu kesho yake akarudi Dom?"

"Hapana Eddy, mwenyewe utaona kwenye email yako, safari zote huwa zinaachana. Inaonekana jamaa Dodoma ni kazini, halafu Dar ni nyumbani kwake. Dodoma hukaa wiki nzima, halafu Dar es Salaam siku mbili au tatu."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# ONYANGO: AZAM MCHAWI WA SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

BEKI wa Simba, Joash Onyango amesema kufanya vibaya kwa timu yake msimu huu kumechangiwa sana na Azam FC kwa kupoteza mechi zote mbili muhimu walipokutana nao.

**Onyango raia wa Kenya pia amekanusha taarifa kuwa baada ya mechi dhidi ya Wydad Athletic Club ya Casablanca nchini Morocco aliandika barua ya kuondoka kwenye klabu hiyo, na wala hana taarifa za kutakiwa na klabu yake ya zamani, Gor Mahia.**

Akizungumza jijini Dar es Salaam, beki huyo aliyesajiliwa na Simba kutokea Gor Mahia ya Kenya mwaka 2019 alisema mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara ya mzunguko wa kwanza dhidi ya Azam walipofungwa bao 1-0 iliwaondoa kwenye reli ya kuwania ubingwa, lakini pia mechi ya nusu fainali ya Kombe la FA dhidi ya timu hiyo hiyo ilipofungwa mabao 2-1, iliwachanganya zaidi na kuhitimisha mwisho wao wa kutoka bila kombe lolote msimu huu.

"Mechi hii ya majuzi tuliyotolewa na Azam kwenye nusu fainali Kombe la FA haikuwa picha nzuri kwetu wachezaji, ilituuma sana, kwa sababu ndiyo nafasi tuliyokuwa tumebaki nayo angalau na sisi msimu huu tupate kombe, na kwenye Ligi Kuu pia tulipopoteza mechi dhidi ya Azam nayo ndiyo iliyotutoa kabisa kwenye mfumo na kwenye reli na hasa mbio za kuwania ubingwa, kwa hiyo niseme hizi mechi mbili tulizocheza nao zimetufanya tupoteze mataji msimu huu," alisema Onyango.

Mechi ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu kati ya timu hizo ilichezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Oktoba 27, Azam ikishinda bao 1-0, lililofungwa na Prince Dube na ile ya nusu fainali ya Kombe la FA, ilichezwa Uwanja wa Nangwanda Sijaona, Mtwara, Mei 7, Simba ikipoiteza kwa mabao 2-1 ya Dube na Lusajo Maikenda, Sadio Kanoute akiifungia timu hiyo bao la kufutia machozi.

Pia Beki huyo wa kati anayeichezea pia timu ya taifa ya Kenya, Harambee Stars alinanusha taarifa kuwa aliandika barua ya kuondoka kwenye klabu hiyo baada ya mechi dhidi ya Wydad Casablanca.

"Binadamu huwezi kumzuia kusema, hata maiti inasemwa, yaani kuna mtu anaonekana kunifahamu mimi zaidi kuliko ninavyojifahamu, mambo yamekuwa mengi sana, mara nimesema hili, lakini mimi sikuwahi kutoa taarifa yoyote ya kuondoka, maana baada ya mechi na Wydad nikasikia maneno mengi, eti naomba kuondoka, si kweli, mimi bado nina mkataba wa Simba, mabosi wenyewe kama wataamua kuvunja sawa, sijasaini kuichezea maisha, huu ni mkataba tu, unaweza kuvunjwa, na kama ukiisha ukiongezwa sawa tu," alisema.



Vijana wakicheza mpira wa Kikapu katika viwanja vya Jakaya Kikwete (JMK Park), jijini Dar es Salaam jana.
**PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mabondia 20 kuzipiga Juni 30

**Na Saada Akida**

MABONDIA 20 wanatarajia kupanda ulingoni katika mapambano ya utangulizi kuelekea katika pambano la Seleman Kidunda dhidi ya Eric Mukadi linalotarajiwa kupigwa Juni 30, mwaka huu kwenye Ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam.

Mbali ya Kidunda ambaye atacheza na Mukadi kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo( DRC), Mfaume Mfaume atapanda ulingoni kupigana na Mkululeko Mhlongo raia wa Afrika Kusini.

Akizungumza na Nipashe jana, promota wa pambano hilo kutoka PAF Promotion Company Limited, Fadhili Maogola alisema maandalizi yanaendelea vizuri ambapo watakuwa na jumla ya mapambano kumi yatakayowakutanisha mabondia 20 wakiwemo watatu kutoka nje ya mipaka ya Tanzania.

"Kwanza tunashukuru Mungu maandalizi ya pambano letu la 'Hata usipo lala pata kucha' yanaendelea vizuri na matarajio yetu ni kuona tunaenda kuijaza Mlimani City kwa kushuhudia pambano kubwa ndani ya mwaka huu ambalo litajumuisha mabondia wengi wakubwa.

"Mapambano nane yatakuwa ya utangulizi ambayo yatakuwa na mabondia 16 kabla Mfaume Mfaume 'Mapafu ya Mbwa' kukamilisha pambano la tisa la utangulizi na kisha Seleman Kidunda kufunga dimba na Mukadi," alisema Maogola.

Aliongeza mapambano hayo ya utangulizi bondia Fadhili Majiha 'Stopper' atapanda ulingoni dhidi ya Jamal Kunoga wakati Saleh Kasim atazipiga na Said Bwanga kabla ya Deo Samweli kumvaa Adam Ngange.

Wengine ni Pius Mpenda ambaye atacheza na Simon Tichecha wa Malawi wakati Rama Jonh Cina akitarajia kupasuana na Yona Segu, lakini Omary Maulid atapanda na Shaban Kibiriti na Boniface Seguda atacheza na Hamza Mahamoudu huku Herry Rashid akitarajia kumalizana na Hussein Pendeza.

## Kipanga FC yatoa neno kwa Fei Toto

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la ufundi la timu ya Kipanga FC ya Zanzibar limemtaka mchezaji wa Azam FC, Feisal Salum Fei Toto kuonesha kile alichokuwa anakifanya kwenye klabu yake ya zamani ili atimize malengo yake.

Akizungumza na Nipashe Kocha Mkuu wa timu ya Kipanga, Hamis Hassan alisema ni wakati wa Fei Toto kuonesha ubora wake msimu ujao.

"Namshauri Feisal asiwe mtu wa kuongea sana kwenye mitandao ya kijamii bali aende akafanye alichoahidi mashabiki wake atakapoanza kuichezea Azam FC," alisema Hassan.

Kocha huyo aliupongeza uongozi wa Klabu ya Yanga kwa busara waliyoitumia kwa kuamua kumuachia mchezaji huyo kwenda kuitumikia timu aliyokuwa anaitaka kipindi kirefu.

"Nimeshukuru kuona suala hili limemalizika salama na Yanga wametumia busara hivyo tumuache kijana kwa sasa atulize akili yake ajipange kwa ajili ya msimu ujao, alisema Kocha huyo.

Alisema Feisal ni mchezaji mzuri ambaye kila Kocha anatamani kufanya naye kazi kutokana na ubora aliokuwa nao na kudai anajua kutumia vema nafasi yake akiwa uwanjani.

Feisal amesaini mkataba wa miaka 3 kuitumikia Klabu ya Azam FC hapo juzi baada ya Yanga kuifanyia kazi kauli ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan ambaye aliwataka waumalize mgogoro waliokuwa nao.

## Mtibwa yaipongeza Bodi ya Ligi

**Na Abdallah Mataka**

MSEMAJI wa klabu ya Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru ameipongea Bodi ya ligi kuu Tanzania Bara (TPLB) , kwa kusimamia vyema ligi hiyo msimu huu wa 2022/2023 ambao umefika tamati jana.

Kifaru ameliambia gazeti hili kwamba, msimu huu uliomalizika umekuwa bora sana kuwahi kutokea.

"Lazima niwape pongezi Bodi ya Ligi kwa maana wamefanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha ligi yetu inaendeshwa kwa kuzingatia kanuni ambazo klabu zote zilitakiwa kuzifuata," alisema Kifaru.

Aliongeza: "Bodi ya ligi wamefanya kazi kubwa sana kanuni zilikuwa zinafuatwa kama zilivyopangwa bila kuangalia uzito wa timu kila aliyefanya makosa ambayo yalihitaji adhabu bodi haikusita kuchukua hatua, hiyo imeleta chachu nzuri sana kwenye Ligi."

Kifaru aliongeza kuwa licha ya changamoto ndogo ndogo ambazo zilikuwa zinajitokeza haziwezi kuwa sababu ya kutowapongeza kwani hizo ni zinaweza kurekebishika.

Aidha kifaru amewashukuru wapenzi na mashabiki wa Mtibwa kwa kuiunga mkono timu hiyo tangu msimu wa ligi ulipoanza hadi kufikia tamati, kwani waliuwa nao pamoja kwenye kila mechi.

"Nitakuwa sijawatendea haki kama sitatoa shukrani zangu za dhati kwa mashabiki na wapenzi wa Mtibwa Sugar wamekuwa pamoja na sisi kila wakati kila tulipopita katika vikwazo hawakutuacha."

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

**RICE NA ARSENAL**
KLABU ya Arsenal itaongeza juhudi za kumnunua Declan Rice kwa pauni milioni 92 kwa matumaini kwamba kiungo huyo wa West Ham na England mwenye umri wa miaka 24 anaweza kujiunga kwa wakati kabla ya kuanza kwa msimu. (***Telegraph***)

**WEST HAM YATAKA NYOTA**
KLABU ya West Ham imepania kumleta kiungo mkabaji wa Fulham na Ureno, Joao Palhinha mwenye umri wa miaka 27, kuchukua nafasi ya Declan Rice, huku nyota wa Manchester City na England, Kalvin Phillips na kiungo wa kati wa Southampton na England, James Ward-Prowse pia wakiwa kwenye orodha hiyo. (***Mail***)

**CHELSEA INAMTAKA**
CHELSEA pia huenda ikawania kumsajili Declan Rice pamoja na kiungo wa kati wa Brighton na Ecuador, Moises Caicedo mwenye umri wa miaka 21. (90min)

**THURAM HUYO LIVER**
NYOTA wa Nice na Ufaransa, Khephren Thuram mwenye umri wa miaka 22, amekubaliana kwa maneno na Liverpool. (***Football Transfers)***

**KOVACIC HUYO CITY**
KIUNGO wa kati wa Chelsea na Croatia, Mateo Kovacic mwenye umri wa miaka 29, amekubali maslahi binafsi na Manchester City baada ya kupiga hatua katika mazungumzo ya usajili. ***(Fabrizio Romano***)

**KONE AWINDWA**
LIVERPOOL imepanga mazungumzo na wawakilishi wa kiungo wa Borussia Moncheng-ladbach, Manu Kone mwenye umri wa miaka 22. (***Fabrizio Romano)***

**KANE NA REAL MADRID**
REAL Madrid inafanyia kazi dau la kutaka kumsajili mshambuliaji wa England, Harry Kane kwa takribani pauni milioni 68 huku mwenyekiti wa Tottenham Hotspur, Daniel Levy akikataa kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 kwa Manchester United. (***Marca***)

**NEWCASTLE KUZOA NYOTA**
KLABU ya Newcastle inatafakari uwezekano wa kuwasajili wachezaji kutoka kwa timu zilizoshushwa daraja katika Ligi Kuu ya England akiwemo kiungo wa Leeds United na Marekani, Tyler Adams mwenye umri wa miaka 24, na winga wa Leicester City, Harvey Barnes mwenye miaka 24 na kiungo James Maddison mwenye miaka 26. (***Telegraph***)

**PSG YAJITOSA KWA GUNDOGAN**
MABINGWA wa Ufaransa, Paris St-Germain wanamtaka kiungo wa kati wa Manchester City na Ujerumani, Ilkay Gundogan mwenye umri wa miaka 32.(***Mail***)

**MAHREZ ATAKIWA ARABUNI**
KLABU ya Al Ahli ya Saudi Arabia imeelezea nia yake ya kutaka kumsajili winga wa Algeria , Riyad Mahrez mwenye umri wa miaka 32 kutoka Manchester City. (***Fabrizio Romano)***

**RAYA DAU JUU**
KLABU ya Tottenham Hotspur inahitaji kuongeza dau lao la pauni milioni 20 kama inataka kumsajili golikipa wa Hispania, David Raya, huku Brentford ikiwa tayari kukataa ofa ya chini ya pauni milioni 40 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27. ( ***Sport)***.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MAN CITY, INTER FAINALI YA KIBABE

## ●●● Zinakutana leo kwenye Ligi ya mabingwa Ulaya, huku Guardiola akipewa...

**INSTANBUL,** Uturuki

MANCHESTER City imefanikiwa kupata mataji matano ya Ligi Kuu ya England, mawili ya FA na manne ya EFL katika zama za Pep Guardiola na sasa itakuwa na nia ya kuongeza taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati leo itakapocheza na Inter Milan mjini Istanbul nchini Uturuki.

**Guardiola alishinda Ligi ya Mabingwa Ulaya mara mbili akiwa na Barcelona lakini amejaribu mara sita katika mashindano hayo akiwa na Man City, ikiwa ni pamoja na kufungwa 1-0 na Chelsea kwenye fainali ya mwaka 2021.**

Kocha wa Inter, Simone Inzaghi, hajawahi kucheza fainali ya Ligi ya Mabingwa akiwa mchezaji au kocha, lakini pia anawinda taji la tatu msimu wa 2022-23, baada ya kuiwezesha Inter kutwaa ubingwa wa Supercoppa Italiana na Coppa Italia.

Nathan Ake alirejea kama mchezaji wa akiba katika fainali ya Kombe la FA na kuwafanya Man City sasa kutokuwa na majeruhi yoyote kuelekea mchezo wa leo.

Inter hawatakuwa na Dalbert (aliyeumia goti), kuna mashaka kama Henrikh Mkhitaryan (anayesumbuliwa na misuli) na Joaquin Correa (misuli) kama wataweza kucheza.

Milan Skriniar kwa upande wake, hajacheza tangu Machi kutokana na jeraha la mgongo.

**TAKWIMU**

Man City hawajafungwa katika Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu wakiwa wameshinda mechi saba na sare tano hadi sasa.

Wameshinda mechi 19 kati ya 23 zilizopita na wamefunga katika mechi 25 mfululizo na walipoteza 1-0 ugenini kutoka kwa Brentford katika mechi yao ya mwisho ya msimu wa Ligi Kuu.

Inter hawajaruhusu bao katika mechi tano kati ya sita za hatua ya mtoano wa Ligi ya mabingwa Ulaya.

**UTABIRI**

Kuelekea mchezo huo jijini Istanbul Man City wanapewa nafasi zaidi dhidi ya Inter kwani staili yao ya uchezaji hasa kwa mashambulizi ya kushitukiza.

City wanahitaji kumtazama kwa karibu fowadi wao wa zamani Edin Dzeko, ambaye aliwafungia mabao 72 katika kipindi cha miaka minne kati ya Januari 2011 na Mei 2015, huku Lautaro Martinez pia akiwa hatari anapopewa nafasi ya kufunga.

Hata hivyo, kikosi cha Guardiola kinafahamu vyema kukabiliana na wapinzani waangalifu.

Inter wamefunga bao la kwanza katika mechi zote tatu za hatua ya mtoano na kuonyesha utulivu mkubwa wakati wa kulinda bao.

Lakini wamekuwa na ushawishi mdogo walipotakiwa kutoka nyuma na kulala kwa mabao 2-0 dhidi ya Bayern Munich katika hatua ya makundi.

Nguvu za City za kupona zimeimarika baada ya kuruhusu bao la kwanza katika ushindi wa hatua ya makundi nyumbani dhidi ya Borussia Dortmund (2-1) na Sevilla (3-1).

Pia walitoka nyuma na kutoka sare ya 1-1 katika mchezo wao wa nusu fainali, mkondo wa kwanza wakiwa na Real Madrid.

City wamefunga mabao matatu au zaidi katika mechi sita kati ya 12 za Ligi ya Mabingwa Ulaya na mafanikio mengine ya juu yanaonekana kuwezekana.

# Arsenal kumuuza Jorginho

**LONDON,** England

ARSENAL ipo tayari kusikiliza ofa kwa kiungo Jorginho msimu huu wa joto, kwa mujibu wa 90min.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 alihamia Uwanja wa Emirates Januari huku Mikel Arteta akitafuta kukichangamsha kikosi chake kuelekea ubingwa wa Ligi Kuu.

Kikosi cha kina kimekuwa tatizo kwa Mhispania huyo, ambaye alitegemea sana mastaa kama Thomas Partey, Granit Xhaka na Martin Odegaard katika miezi mitano ya kwanza ya msimu, na uzoefu wa Jorginho wa kushindana katika kiwango cha juu ulionekana kama nyongeza ya kukaribishwa..

Hata hivyo, usajili wa Jorginho ulionekana kama hatua ya muda mfupi tu na inaelewa kwamba Arsenal haitamzuia msimu huu wa joto ikiwa atapata nafasi ya kurejea Italia.

Kocha wa zamani wa Chelsea, Maurizio Sarri, ambaye sasa anainoa Lazio, ana nia ya kuungana tena na Jorginho kwenye Uwanja wa Olimpico, huku pia Napoli na AC Milan zimeonesha nia ya kumtaka.


Arsenal hawataki kumlazimisha Jorginho kuondoka katika klabu hiyo lakini wanafahamu kabisa kwamba wanahitaji kutengeneza nafasi kwenye kikosi chao kwa ajili ya wachezaji wanaoingia.

Granit Xhaka anaondoka katika klabu hiyo na kujiunga na Bayer Leverkusen na Albert Sambi Lokonga, ambaye muda wake wa mkopo katika klabu ya Crystal Palace haukufaulu, pia huenda akatolewa.

Kuondoka kwao kunaweza kurahisisha kuwasili kwa Declan Rice na Moises Caicedo, huku Arsenal wakiwa na nia ya kusajili wachezaji wote wawili licha ya bei zao za juu.

Nahodha wa West Ham, Rice, ambaye alinyanyua taji la Europa Conference Jumatano usiku, anataka kusonga mbele ili kutimiza malengo yake lakini klabu hiyo itashikilia msimamo wao wa dau la pauni milioni 100.

Kwa upande wa Brighton, wanaweza kuwa tayari kukubali takriban pauni milioni 80 kwa Caicedo – fedha ambayo Arsenal hawakuwa tayari kuitoa Januari.





# MAC ALLISTER AJIFUNGA MIAKA MITANO LIVERPOOL

**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL imekamilisha dili la pauni milioni 35 kumsajili kiungo, Alexis Mac Allister kutoka Brighton kwa mkataba wa miaka mitano.

Ada inaweza kupanda hadi pauni milioni 55 kwa kiungo huyo wa Argentina, ambaye aliisaidia Brighton kumaliza nafasi ya sita kwenye Ligi Kuu ya England msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 alifunga mabao 20 katika mechi 112 akiwa na Seagulls hao na kuisaidia Argentina kushinda Kombe la Dunia la 2022.

"Ni ndoto iliyotimia na siwezi kusubiri," alisema Mac Allister.

"Nilitaka kuwa ndani tanu siku ya kwanza ya maandalizi ya msimu mpya, kwa hiyo ni vizuri kwamba kila kitu kimekamilika. Ninatazamia kukutana na wachezaji wenzangu.

"Ulikuwa mwaka mzuri kwangu - Kombe la Dunia, kile tulichofanikiwa na Brighton - lakini sasa ni wakati wa kufikiria juu ya Liverpool na kujaribu kuwa mchezaji bora na mwanadamu bora kila siku."

Kocha wa Liverpool Jurgen Klopp anatazamia kuimarisha safu yake ya kiungo huku James Milner, Naby Keita na Alex Oxlade-Chamberlain wakiondoka Anfield msimu huu wa joto.

Walikuwa wamepunguzwa bei kutokana na uhamisho wa nyota wa Borussia Dortmund, Jude Bellingham, ambaye anaelekea kujiunga na Real Madrid baada ya klabu hizo kukubaliana ada ya euro 103.

Mac Allister alijiunga na Brighton kutoka Argentinos Juniors Januari 2019 na mara moja akarejea katika klabu hiyo ya jijini Buenos Aires kwa mkopo.

Ameichezea Argentina mara 16 na kuibuka kama mchezaji muhimu wakati wakitwaa taji lao la tatu la Kombe la Dunia Desemba.

# Neymar atajwa kutua Saudi Arabia

**PARIS,** Ufaransa

WAWAKILISHI wa Neymar wamefanya mazungumzo juu ya uwezekano wa kuhamia Saudi Arabia, kwa mujibu wa 90min, huku uwezekano wa kurejea Barcelona kumekataliwa na kocha Xavi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 amebakiza miaka miwili katika mkataba wake na Paris Saint-Germain, huku miamba hao wa Ligue 1 wakiwa na chaguo la kuongeza kwa miezi 12 zaidi.

Lakini Mbrazil huyo mwenye amekuwa akilengwa na baadhi ya mashabiki wa PSG ambao wanachukizwa na uchezaji wake uwanjani na hivi karibuni kulikuwa na maandamano nje ya nyumba yake wakimtaka aondoke katika klabu hiyo msimu huu wa joto.

90min ilifichua mwanzoni mwa Mei kwamba wamiliki wa Newcastle walikuwa wakitafuta uwezekano wa kumchukua Neymar kwenda.

Hata hivyo, vyanzo vimethibitisha kwa 90min kwamba mazungumzo yamefanywa na wawakilishi wa Neymar na wajumbe wanaowakilisha Ligi ya Saudi Pro, ambao wana nia ya kumfanya atue huko Mashariki ya Kati.

Karim Benzema alijiunga na Al Ittihad akitokea Real Madrid kwa mkataba wa miaka mitatu Jumanne, huku N'Golo Kante na wachezaji wengine wakipewa fedha nyingi kufuata nyayo za Cristiano Ronaldo aliyejiunga na Al Nassr mwisho wa 2022 ili kuipandisha Saudi Arabia katika umaarufu wa soka.

90min inaelewa kuwa Neymar amepewa ofa ya kwenda Barcelona - ambao walikosa kumsajili tena Lionel Messi baada ya kuchagua kujiunga na Inter Miami - lakini kocha Xavi alikataa nia ya kumsajili tena, akikimbia kituo cha Twitch kuhusu uvumi huo: "Nimeshangaa... hayuko katika mpango wetu.

"Nampenda sana Ney kama rafiki, lakini tuna vipaumbele tofauti."

Hapo awali Neymar alitumia misimu minne iliyosheheni mataji Camp Nou kati ya 2013 na 2017, akishinda mataji matatu mwaka 2015, kabla ya kufanya uhamisho wa rekodi ya dunia wa euro milioni 222 kwenda PSG.

Ameshinda orodha ya mataji ya Ligue 1 katika mji mkuu wa Ufaransa, lakini hajaweza kuisaidia PSG kushinda taji la kwanza la Ligi ya Mabingwa Ulaya licha ya kucheza pamoja na Messi na Kylian Mbappe kwa misimu miwili iliyopita.

Muda mwingi wa Neymar akiwa Paris amekuwa nje ya uwanja akiwa majeruhi, huku maradhi mbalimbali yakimfanya kucheza mechi 112 pekee za Ligue 1 ndani ya misimu sita kamili klabuni hapo.

Manchester United na Chelsea pia zimeonesha nia ya kumtaka Neymar.



# WAJIKI SASA WAELEKEZA NGUVU KWENYE JOGGING

Na Sabato Kasika

SHIRIKA la Jitihada la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI) la jijini Dar es Salaam, limeelekeza kampeni zake za kupinga rushwa ya ngono katika makundi ya mchezo wa jogging.

Mkurugenzi wa WAJIKI, Janeth Mawinza aliliambia gazeti hili jijini Dar es Salaam jana kuwa shirika hilo limepanua kampeni zake, kwa kuwa rushwa ya ngono imesambaa.

**"Awali tulikuwa tukiendesha kampeni ya 'Safari Salama Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana', katika vijiwe vya madereva wa bodaboda, bajaj, daladala, shuleni na mitaani," alisema Janeth.**

Alifafanua kuwa wapo baadhi ya wadau ambao wameunga mkono kampeni hizo, wakiwamo vijana wa makundi ya jogging ambao sasa WAJIKI inafanya nao kampeni ya kupiga vita rushwa hiyo.

"Baada ya kupata wadau hao, sasa kampeni yetu inaitwa Unga Tela Vunja Ukimya, Safari Salama Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana'," alisema.

Alisema hata katika makundi ya jogging, kuna rushwa ya ngono kwa kuwa mchezo huo unahusisha jinsi zote, na kwamba kupitia kampeni hiyo kunaweza na matokeo chanya.

"Ninaamini kwamba kupitia ufadhili huu wa Women Fund Tanzania (WFT), lengo la kutaka jamii yote inakuwa na uelewa kuhusu madhara ya rushwa ya ngono na ukatili wa kijinsia kwa ujumla linaweza kufikiwa," alisema.

Janeth alisema tayari wameshafanya kampeni na makundi ya jogging ya Tabata na Kinondoni, huku wakiwa na mabango yenye ujumbe wa kuhamasisha vita dhidi ya ukatili huo.



Vijana wa Smart Jogging wa Tabata jijini Dar es Salaam wakifanya mazoezi ya viungo hivi karibuni. Wao ni miongoni mwa makundi yanayoshirikiana na WAJIKI katika kampeni ya kupinga ruhwa ya ngono. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mayele, Saido jino kwa jino



INATOKA UK 24

Mbeya City rasmi sasa itacheza mchezo wa Play Off kuwania kubaki ligi kuu baada ya jana kukubali kipigo cha bao 1-0 kutoka KMC, Dodoma jiji ikiwa nyumbani kwa Ruvu Shooting ilifanikiwa kupata ushindi wa bao 1-0, Mtibwa Sugar wakiwa nyumbani Manungu walipata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Geita Gold, Ihefu wakiwa nyumbani walipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Kagera Sugar.

Pamoja na kushinda bao 1-0, Uwanja wa Nelson Mandela, Sumbawanga, KMC italazimika kucheza mechi ya mchujo dhidi ya timu hiyo hiyo iliyocheza nayo jana, Mbeya City.

KMC imemaliza ligi ikishika nafasi ya 13 na pointi zake 32, Mbeya City ikiwa kwenye nafasi ya 14 kwa pointi 31, baada ya kupoteza mechi ya jana, hivyo zitalazimika kucheza tena mechi mbili za nyumbani na ugenini kwenye 'play off'.

## Mashindano ya Karate kurindima

Na Shufaa Lyimo

MASHINDANO ya mchezo wa Karate yanatarajiwa kufanyika Juni 17 hadi 18 mwaka huu kwenye ukumbi wa shule ya Sekondari Mwenge mkoani Singida.

Akizungumza na gazeti la Nipashe jana, Msemaji wa Chama cha Karate Tanzania, Salha Abdallah alisema lengo la mashindano hayo ni kupata wachezaji watakaounda timu ya Taifa pamoja na kuuhamasisha mchezo wa karate mikoani.

"Lengo la mashindano hayo ni kuhamasisha wadau mbalimbali mikoani wafahamu jinsi ya kucheza huu mchezo ikiwemo kuangalia viwango vya kila mchezaji," alisema Abdallah.

Msemaji huyo alisema mashindano hayo yatashirikisha Klabu 19 kutoka mikoa ya Tanzania Bara pamoja na Visiwani Zanzibar.

Aliitaja baadhi ya mikoa itakayotoa timu zao kuwa ni Arusha, Mbeya, Dar es Salaam Iringa, Njombe, Ruvuma, Morogoro pamoja na mwenyeji wa mashindano Singida.

Alisema kwa upande wao wanaendelea na mazoezi kuhakikisha wanakwenda kufanya vema na kuwataka wadau mbali mbali wajitokeze kwa wingi siku hiyo.

Aidha alisema anafurahi kuona mchezo huo unapendwa na watu wengi tofauti na ulivyokuwa miaka iliyopita.

## Waarabu wampandia dau Mayele

INATOKA UK 24

mtoa taarifa.

Mayele alipotafutwa na Nipashe alisema: "Siwezi kusema jambo lolote juu ya hatima yangu ya kubakia Yanga kwa sasa hadi msimu utakapokuwa umemalizika, nataka kuweka nguvu yangu kwenye mechi zilizobaki ligi na fainali ya Kombe la FA na baada ya hapo ndiyo naweza kujua kama nitaondoka au nitabakia Yanga."

Rais wa Yanga, Injia Hersi Said tayari alishaweka wazi juu ya mchezaji yoyote kama atatakiwa na timu nyingine wampe machaguo matatu ikiwemo kumboreshea maslahi ya mkataba wake huku akisisitiza hawatokuwa tayari kuzuia mchezaji yeyote ambaye atakuwa amepokea masilahi mazuri.

# Michezo

Nipashe

Jumamosi Juni 10, 2023




UK. 22

**Neymar atajwa kutua Saudi Arabia**




Wachezaji wa Yanga wakishangilia na kombe lao baada ya kukabidhiwa jana kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya. PICHA: **FAUSTINE FELICIANE**

## Waarabu wampandia dau Mayele

**Na Saada Akida**

MIAMBA ya soka nchini Saudi Arabia ina mpango wa kuibomoa Yanga baada kuweka ofa mezani ya kuhitaji saini ya mshambuliaji wao kinara, Fiston Mayele.

Mayele ambaye msimu huu amekuwa na mafanikio makubwa katika timu hiyo akifanikiwa kuibuka mfungaji bora wa michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika kwa kufunga mabao saba huku akisaidia timu yake kucheza fainali ya michuano hiyo ambayo ilishindwa kuutwaa ubingwa mbele ya USM Alger.

Msimu huu katika Ligi Kuu Bara, mshambuliaji huyo amefanikiwa kufunga mabao 16 na kuiwezesha Yanga kutetea ubingwa huo.

Taarifa za uhakika kutoka kwa watu wa karibu na mshambuliaji huyo zinasema kuwa Mayele amepokea ofa nyingi za kutoka nje ya mipaka ya Tanzania ikiwemo AL Qadisiyah, kwa nia ya kutaka saini yake kuelekea katika msimu ujao wa ligi.

Chanzo hicho kilisema kwamba, Klabu ya Al Qadisiyah ambayo anacheza Simon Msuva na Walter Bwalya, wamepewa taarifa zake.

"Nadhani kila mtu anajua kwamba Mayele kubakia Yanga msimu ujao ni jambo gumu kutokana na mafanikio ambayo ameyapata msimu huu na ukiangalia aliyempeleka Msuva kule Saudi Arabia ndiyo anayemsimamia Mayele," alisema

INAENDELEA UK 23

# Mayele, Saido jino kwa jino

**Walingana kwenye ufungaji bora Ligi Kuu, Kamati ya tuzo kuamua..**

**Adam Fungamwango na Faustine Feliciane,** MBEYA

WAKATI Simba na Yanga zikimaliza msimu wa ligi kwa ushindi kwenye mechi zao za mwisho, vita ya ufungaji bora imeishia kwa wachezaji Fiston Mayele wa Yanga na Saido Ntibazonkiza kulingana kwa magoli kila mmoja akifunga 17.

**Kabla ya michezo ya jana, Mayele alikuwa mbele akiwa na magoli 16 akifuatiwa na Ntibazonkiza akiwa na mabao 15 na wote walikuwa wakisaka nafasi ya kuongeza mabao kujihakikishia kutwaa tuzo ya mfungaji bora msimu huu.**

Nyota hao walifanikiwa kufunga kila mmoja Mayele akifunga bao moja kwenye ushindi wa Yanga wa mabao 2-0 dhidi ya Tanzania Prisons kwenye uwanja wa Sokoine mjini hapa na Ntibazonkiza akifunga mabao mawili kwenye ushindi wa Simba wa mabao 3-1 dhidi ya Coastal Union.

Kwa mujibu wa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya ligi, Almas Kasongo, kamati ya tuzo itaamua na kutangaza nani atapewa tuzo ya mfungaji bora msimu huu kati ya Mayele na Ntibazonkiza.

"Suala la tuzo hilo litaamuliwa na kamati maalum ya tuzo, wanafahamu nani anastahili, kwa hiyo tusubiri tuone nini watasema," alisema Kasongo muda mfupi baada ya mchezo wa Yanga dhidi ya Tanzania Prisons kumalizika jijini Mbeya.

Vita ya kuwania kiatu cha dhahabu iliibuka ghafla, kwani Jumanne iliyopita, Saido alifunga mabao matano kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, Simba ikipata ushindi wa mabao 6-1 dhidi ya Polisi Tanzania na kufikisha idadi hiyo ya mabao ambapo iliwalazimu mabosi wa Yanga kumsafirisha Mayele kwenda Mbeya kucheza mechi ya mwisho dhidi ya Prisons na kufanikiwa kufunga bao moja.

Saido, raia wa Burundi alifunga mabao yake mawili dakika ya 14 na 73, akiiwezesha Simba kumaliza ligi kwa kuifunga Coastal Union mabao 3-1, lingine likitiwa kwenye kamba na John Bocco dakika ya 56, bao la machozi la wageni likifungwa kwa mkwaju wa penalti na Amza Moubarack dakika ya saba ya mchezo.

Kwenye Uwanja wa Sokoine Mbeya, Mayele, ambaye kwa muda mrefu alikuwa akiongoza kwenye ufungaji bora, alifunga bao dakika ya 33, akiiwezesha Yanga kuondoka ugenini na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Prisons, lingine likifungwa na Yannic Bangala dakika za mwisho za mchezo.

Baada ya michezo ya jana Yanga walikabidhiwa rasmi ubingwa wa ligi kuu baada ya kumaliza ligi wakiwa na pointi 78 wakifuatiwa na Simba wenye pointi 75.

Matokeo mengine Azam aliitandika Polisi Tanzania mabao 8-0 na hivyo kuipa mkono wa kwaheri timu hiyo ambayo imeshuka rasmi daraja, Namungo wakiwa nyumbani uwanja wa Majaliwa walilazimishwa sare ya bao 1-1 na Singida United.

INAENDELEA UK 23


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >